




**Mahakama** Kuu kusikiliza kesi mbili za Freeman Mbowe leo na kesho

UKURASA 4


# Nipashe

Jumatatu Agosti 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580688

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Allegri aitaka Juve kumsahau Ronaldo wakati ikila kichapo**

UKURASA 20

# Gwajima, tozo miamala ya simu kutikisa Bunge

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MCH. MIEZI 18 JELA, FAINI YA MIL. 3/- KUKATAA KUPELEKA WATOTO SHULE

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera, imemhukumu mchungaji Merchades...

UKURASA WA 3

### BUNGE LABAINI UTATA MKATABA WA ATCL, TGFA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imebaini kuwapo na utata mkubwa kwenye mkataba...

UKURASA WA 5

### UKAGUZI VYAMA VYOTE VYA SIASA KUANZA LEO

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imesema inaanza leo kufanya ukaguzi kwa vyama vya siasa huku...



Rais Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuzindua ofisi ya maendeleo Kata ya Kizimkazi Dimbani na nyumba mbili za madaktari zilizojengwa kwa ufadhili wa Benki ya CRDB na kugharimu Sh. milioni 300. Wengine ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman (wanne kulia), Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Hussein Laay (wapili kushoto), Mwenyekiti wa CRDB Bank Foundation, Martin Warioba (watatu kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wapili kulia). **NA MPIGAPICHA WETU**

## Hatimaye Hamza azikwa Dar



UKURASA 2



Mwenyekiti wa kamati ya waliokuwa wakazi wa Magomeni Kota, George Abel, akizungumza na wakazi hao wa eneo hilo, Dar es Salaam jana kutokana na kuwapo kwa habari za kutatanisha juu ya baadhi yao kutokurudishwa katika majengo mapya yaliojengwa na serikali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Magomeni Kota wamlilia Samia kupigwa kalenda makazi

UKURASA 5

MICHEZO NDAYIRAGIJE AAHIDI KUIPAISHA GEITA UK.23 MAONI, KATUNI UK.6

# Gwajima, tozo miamala ya simu kutikisa Bunge

**Na Sanula Athanas**

MKUTANO wa Nne wa Bunge la 12 unatarajiwa kuanza kesho jijini Dodoma huku tuhuma za kushusha hadhi na heshima zinazowakabili wabunge wawili wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Askofu Josephat Gwajima na Jerry Silaa zikitarajiwa kuwa sehemu ya mambo yatakayotikisa.

Mbali na tuhuma dhidi ya wabunge hao wa Kawe na Ukonga, mtawalia, sakata la tozo za miamala ya simu linatarajiwa kuwa sehemu ya hoja zitakazoibuliwa wakati wa mijadala ya mkutano huo.

Vilevile, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) zitawasilisha taarifa zake kuhusu namna zilivyoshughulikia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

**GWAJIMA, SILAA**

Kwa siku tano mfululizo kuanzia Jumatatu ya wiki iliyopita, wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge waliketi kwa lengo la kuwahoji Askofu Gwajima na Silaa kutokana na tuhuma za kushusha hadhi na heshima ya Bunge zinazowakabili.

Kuhojiwa kwa wabunge hao ni maagizo ya Spika Job Ndugai, aliyeitaka kamati hiyo kuwaita na kuwahoji dhidi ya tuhuma hizo.

Wawili hao walihojiwa mbele ya kamati hiyo, mahojiano yakifanyika kwa siku mbili kwa kila shahidi. Awali kamati ilipanga kuwahoji kwa siku nne lakini ililazimika kuongeza siku moja kutokana na Silaa kushindwa kufika mbele ya kamati katika siku ya pili ya mahojiano.

Kama kamati ikiwakuta na hatia, itapendekeza adhabu dhidi yao ambayo itajadiliwa na Bunge ili ama kuridhiwa au kutoridhiwa. Kuna uwezekano taarifa ya kamati hiyo kuwasilishwa bungeni wakati wa mkutano huo utakaoanza kesho, lakini itategemea uamuzi wa uongozi wa Bunge.

**TOZO ZA MIAMALA**

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha kuwa kesho serikali itaweka hadharani ilichokiamua kuhusu tozo za miamala ya simu baada ya kupokea ripoti ya kamati iliyoundwa kushughulikia suala hilo.

Suala hilo linatarajiwa kuwa sehemu ya hoja zitakazoibuliwa wakati wa mkutano huo wa Bunge, ikizingatiwa tayari Spika Ndugai ameshaweka wazi kuwa Bunge liko tayari kufanya marejeo ya sheria iliyoanzisha tozo hizo.

Huku serikali ikitangaza kukusanya Sh. bilioni 48 katika mwezi wa kwanza wa tozo hizo, wadau wamekuwa wakizipinga vikali kwa kile wanachodai kuongeza ugumu wa maisha kwa wananchi.

Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Catherine Ruge, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam kuwa chama chao hakiungi mkono tozo hizo kwa kuwa zinaumiza wananchi hasa wanawake walioko vijijini ambao wanategemea kwa kiwango kikubwa kufanya miamala ya simu katika kuendesha shughuli zao za ujasiriamali.

**HOJA ZA CAG**

Wakati wa mkutano uliopita wa Bunge (Bunge la Bajeti), Spika Ndugai aliagiza PAC na LAAC kushughulikia hoja zilizoibuliwa na CAG katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu.

Spika Ndugai aliagiza taarifa za kamati hizo ziwasilishwe wakati wa mkutano wa Septemba utakaoanza kesho badala ya mkutano wa Novemba ilivyokuwa imezoeleka awali.

Tayari kamati hizo zimeshawaita na kuwahoji watendaji wa taasisi na halmashauri zilizobainika kuwa na shida kwenye hesabu zake.

**BIMA KWA WOTE**

Juzi mjini Dodoma Msemaji Mkuu wa Serikali, Msigwa, aliwaambia wahariri wa vyombo vya habari kuwa wakati wa mkutano ujao wa Bunge, serikali itawasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na tayari Sh. bilioni 349 zimetengwa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa bima hiyo hata kabla ya kupitishwa kwa sheria yenyewe.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Khamis Hamza Chilo, akizungumza na abiria wanaosafiri kwenda mikoa mbalimbali nchini wakati wa ziara aliyoifanya alfajiri ya jana lengo ikiwa kuwakumbusha wasafiri kupaza sauti waonapo viashiria vya uvunjifu wa sheria za barabarani huku pia akiwaasa kuchukua tahadhari juu ya maambukizi ya UVIKO-19. Ziara hiyo imefanyika katika kituo kikuu cha mabasi Dodoma. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# Hatimaye Hamza azikwa Kisutu Dar

**Na Elizabeth Zaya**

MKAZI wa Jiji la Dar es Salaam, Hamza Mohammed (34) anayedaiwa kufanya shambulio la kuwapiga risasi na kuwaua askari wa Jeshi la Polisi jijini Dar es Salaam, hatimaye alizikwa jana.

Hamza anayedaiwa kufanya tukio hilo katika makutano ya barabara ya Kinondoni na Kenyatta Drive, alizikwa katika makaburi ya Kisutu majira ya jioni.

Hamza ambaye alizua gumzo baada ya kuwaua askari watatu pamoja na askari wa kampuni ya ulinzi kisha naye kuuawa muda mfupi, baada ya Sara ya Magharibi katika makaburi hayo.

Kabla ya kuzikwa kwa Hamza, tayari Jeshi la Polisi kupitia Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, lilitoa ruhusa ya ndugu wa Hamza kwenda kuuchukua mwili na kuendelea na shughuli za mazishi.

IGP Sirro alisema: "Mwili wa Hamza tutawakabidhi ndugu zake kwa sababu sisi tayari tumeshaufanyia kazi, kama ndugu zake wanataka kuja kuuchukua wafanye hivyo lakini siku zikipita hawajaja kuuchukua, halmashauri itakwenda kuuzika."

Maandalizi ya sehemu ya kuzika mwili wa Hamza yalianza mapema jana, lakini baadaye lilitolewa tangazo lililoeleza kwamba maziko yatafanyika baada ya Sara ya Magharibi saa moja usiku.

Baadhi ya watu waliomfahamu Hamza enzi za uhai wake wakizungumza katika makaburi ya Kisutu, walisema hawakuamini kama kijana huyo angefanya tukio kama hilo kutokana na namna walivyomfahamu.

Miongoni mwa watu hao ambao pia waliwahi kuishi naye sehemu mbalimbali akiwamo mmoja aliyefahamika kwa jina la Rajabu, alisema Hamza alikuwa ni miongoni mwa watu aliyekuwa anatoa sadaka ya kuwasaidia wenye uhitaji misikitini.

"Nilikuwa namuona huyu kijana akija kwenye msikiti pale Maamur alikuwa ni kijana mchangamfu sana ambaye huwezi kumdhania kama anaweza kufanya tukio kama hili, hata baadhi ya watu wenye uhitaji waliokuwa wakija pale msikiti wakiwa na shida alikuwa anawasaidia hata katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, alikuwa anasaidia sana watu," alisema Rajabu.

Aliongeza: "Tumekunywa naye kahawa sana kwenye kijiwe cha pale fire, alikuwa hana neno, alikuwa hana maneno mengi, alikuwa akichoka anajiondokea tu bila shida, ndiyo maana tuliposikia kwamba amefanya tukio kama hili tulishtuka sana na tulishtuka zaidi kusikia yule bwana siku ya tukio alikuwa kama chizi."

Tukio la Hamza kufanya shambulio na kuwaua askari wa Jeshi la Polisi watatu na mlinzi mmoja wa kampuni ya SGA lilitokea Agosti 25, mwaka huu.

## Waziri Mkuu awahakikishia uhuru wa kuabudu



**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea kusimamia uhuru wa kuabudu kwa kila mwananchi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Amesema kuwa serikali itaendelea kuheshimu uhuru huo wa ibada zinazoendeshwa katika nyumba za dini na itaendelea kushirikiana na taasisi zote za dini na madhehebu yote kwa ajili ya ustawi wa taifa na watu wake.

Amesema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ibada ya kusimikwa kwa Askofu Mkuu wa Muungano wa Makanisa ya Umoja wa Pentekoste Tanzania, Elieza Isaka Mazinge, katika Kanisa la Pentekoste Wilaya ya Nzega mkoani Tabora.

"Pale mtakapopata tatizo lolote linalohitaji kutatuliwa na serikali waoneni viongozi wa serikali walioko katika maeneo yenu, maelekezo ya serikali ni lazima viongozi hao waunge mkono jitihada za dini katika kufanya taifa hili kuwa tulivu."

Akizungumza na waumini wa kanisa hilo, Waziri Mkuu alisema ni muhimu Watanzania kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kujiongezea kipato, kujiletea maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa, kwa sasa Tanzania iko katika uchumi wa kati na mafanikio hayo yametokana na kujitoa na kuchapa kazi kwa Watanzania na kuwataka kuendelea kudumisha amani na kuiunga mkono serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Awali akisoma taarifa ya kanisa hilo, Mazinge alisema kanisa linatambua jitihada za serikali katika kupambana na janga la Uviko-19, hivyo kanisa limechangia mitungi ya oksijeni yenye thamani ya shilingi milioni mbili katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega kwa ajili ya wagonjwa wenye changamoto ya upumuaji.

## HABARI KITAIFA



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi (katikati), akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Bunge wakati wa mkutano wa pamoja uliofanyika jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Jane Kajiru na Mwenyekiti wa TUGHE Ofisi ya Bunge, Chacha Nyakega. **PICHA: BUNGE**

# Mchungaji afungwa miezi 18 jela, faini mil. 3/- kukataa kupeleka watoto shule

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera, imemhukumu mchungaji Merchades Mugishagwe, kutumikia kifungo cha miezi 18 na kulipa faini ya shilingi milioni tatu kwa kukataa kupeleka watoto wake shule.

Mchungaji huyo ametiwa hatiani kwa makosa ya matatu ambayo ni kushindwa kutekeleza wajibu wake kama mzazi, kushindwa kupeleka watoto shule na kujihusisha na vikundi visivyotakiwa kijamii.

Hukumu hiyo ilitolewa wiki iliyopita na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Daniel Nyamkerya, ambaye amemhukumu mshtakiwa namba mbili katika kesi hiyo mke wa mchungaji huyo, Agripina Maganja, kifungo cha nje kwa muda wa miezi sita.

Akizungumza mahakamani hapo, Wakili wa Serikali, Grey Uhagile, alisema katika hukumu hiyo mchungaji huyo amehukumiwa adhabu ya miezi sita kwa kila kosa na kwa kuwa atatumikia adhabu hiyo kwa wakati mmoja, atakaa gerezani kwa muda wa miezi sita.

"Kimsingi walikuwa na mashtaka manane, makosa matatu ya mwanzo ni kushindwa kutekeleza majukumu yao kama wazazi chini ya sheria ya mtoto ya mwaka 2009, lakini walishindwa kuwapeleka watoto shuleni wenye umri wa kuanza shule.

Katika kesi hiyo ambayo ilisimamiwa na wakili wa utetezi Rogate Assey, mashahidi wawili kati ya watatu ndiyo walitoa ushahidi kwa upande wa washtakiwa, baada ya shahidi namba tatu aliyetajwa na washtakiwa hao kuwa ni Mungu, kushindwa kufika mahakamani na kusababisha ushahidi wa kesi hiyo kufungwa Agosti 12, mwaka huu.

Mchungaji Mugishagwe na mke wake Agripina, walifikishwa katika mahakama hiyo, Februari mwaka huu, wakikabiliwa na mashtaka manane likiwamo la kushindwa kutimiza wajibu wao kama wazazi kuwapeleka watoto wao watatu shule, wakidai kufanya hivyo ni dhambi, kwa madai maandiko ya Mungu hayaruhusu watoto kwenda shule.

Watoto hao mkubwa ana umri wa miaka 13, wa pili wa kiume miaka tisa na wa tatu wa kike miaka mitano, Februari mwaka huu, walipelekwa shule kwa lazima na serikali na sasa wanaendelea na masomo katika Shule ya Msingi Mugeza Mseto iliyopo katika Manispaa ya Bukoba.

Pia, watoto hao hawajawahi kupelekwa kliniki na wanapougua hawapelekwi hospitali, kadhalika wanafamilia hao hawatazami televisheni wala kusikiliza radio.

Mtu huyo anayejiita mchungaji ameweka kanisa lake nyumbani kwake ambalo halina jina na akiulizwa makao makuu yake hujibu yapo mbinguni.

# Bunge labaini utata mkataba wa ATCL, TGFA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imebaini kuwapo na utata mkubwa kwenye mkataba kati ya Shirika la Ndege nchini (ATCL) na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA).

Imesema ATCL bado wanaendelea kupata hasara na kuitaka serikali kuchukua hatua za kuimarisha utendaji wake, ili uwekezaji huo uwe na faida kwa taifa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu hatua zilizofikiwa na kamati hiyo, baada ya kamati yake kulihoji ATCL na TGFA kufuatia hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

"Mkataba wao na TGFA una utata mkubwa sana kiasi kwamba mwingiliano wao unafanya kamati ya PAC ishindwe kutoa maagizo yoyote hadi tukutane na pande zote husika, yaani Katibu Mkuu Ikulu, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, ATCL pamoja na TGFA, tarehe ya kikao hicho itapangwa siku za hivi karibuni," alisema Kaboyoka.

Alisema: "Tumekataa kupokea vitabu vyao vya hesabu za ATCL na kwa TGFA hatukuwasikiliza kwa sababu walikuja maofisa wanao kaimu tu, Ofisa Masuuli hakuja wala hakuleta barua ya kutokuwapo kwake hivyo tuliwarudisha."

Alipoulizwa kuhusu utata wa mkataba huo alisema: "ATCL wanadai kuwa wanalipa gharama kubwa kwa wakala na hata hela za matengenezo ya ndege zinakuwa na utata mkubwa sana."

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema: "Kulikuwa na makubaliano ya gharama kwamba ndege inapokwenda kwenye D-check basi fedha kiasi fulani kila mwezi kipelekwe TGFA kwa ajili ya utengenezaji wa ndege itakapofika kipindi, lakini ATCL wametengeneza ndege zao moja kwa moja kwa kuingia mikataba wao wenyewe bila kuhusisha TGFA hivyo kuleta hisia kwamba kuna malipo mara mbili."


### KUPOTEA KWA CHETI



**JASETH CHELESTINO NGOLO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1533/0065** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIPONZELO SEKONDARI mwaka 2017**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: IRI/IRI/RB/225905/2020.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FELIX FELICIAN ISMAIL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye namba za usajili **T 380 DCD** chasis namba **SR4001173389** engine namba **3S5138097,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **MBE/TUK/RB/412370/2021**

116429302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe**

**Kituo cha njombe mjini**
**Mkoa wa njombe**

**Usimamizi wa mirathi na 83/2003**

**Anna Mosses Chibwana.........marehemu**

**Leah Mosses Ng'wavi.............,mwombaji**

**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika katika mahakama hii na kuangalia orodha ya mali za marehemu(fomu namba V) na hesabu za mirathi (fomu namba VI) katika jalada la mirathi
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali(fomu namba V) na au hesabu za mirathi (fomu namba VI) hii yawe yameandikishwa katika mahakama hii mnamo au kabla ya siku ya tarehe 06th ya mwezi wa septemba mwaka 2021 mpaka kufikia saa 9:30 alasiri
Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 27th agosti mwaka 2021

**Hakimu Mkazi**

HAKIMU MKAZI NJOMBE - MJINI

116429402

**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

## TENDER CANCELLATION NOTICE

**INVITATION TO BID: No. ITB/21/TZAKA/SUP/001 FOR THE SUPPLY AND INSTALLATION OF MEDICAL STATIC RACKING (SHELVES) FOR THE MEDICAL WAREHOUSE AT UNHCR LOGISTICS BASE, KASULU.**

216429202

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam has cancelled this tender which was accessible in the link below;

**https://drive.google.com/drive/folders/1eQ3OSEopixKYSOP7mDAEmE2StGyqiIUT?usp=sharing**

# ...Ya uhujumu uchumi na ugaidi kunguruma kesho

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kesho inatarajia kuanza kusikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Kesi hiyo ambayo washtakiwa walisomewa maelezo ya mashahidi Agosti 23, mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imepangwa kusikilizwa mbele ya Jaji Elinaza Luvanda.

Upande wa Jamhuri unatarajia kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali dhidi ya mashtaka sita ya ugaidi yanayowakabili.

Katika shauri hilo la uhujumu uchumi namba 16/2021 upande wa mashtaka unatarajia kuita mashahidi 24 akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz.

Jamhuri inawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, Jenitreza Kitali na Esther Martin.

Mbowe na wenzake watatu wanawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Lwekamwa Rweikiza na Marie Mushi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katila Hoteli ya Aishi iliyopo Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa Taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Sabaya.

Shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi

kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamuhuri ya Maungano wa Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi.

Shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastola yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani katika shtaka la sita anadaiwa Agosti 10, mwaka 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa(JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la mvua moja, jacket moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja,sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

Shahidi wa kwanza anatarajia kuwa Kamishna wa Polisi Robert Boaz ambaye katika ushahidi wake uliosomwa Mahakama ya Kisutu anadai Julai mwaka 2020 alipokea simu kutoka kwa mtu asiyemfahamu akamwambia kuna uhalifu umepangwa kufanyika kwa ajili ya kudhuru viongozi wa serikali.

Anadai mtu huyo alijitambulisha kuwa ni Luteni Denis Urio, alimwambia aende ofisini kwake, alienda akampa taarifa kuwa Mbowe anataka amtafutie wanajeshi wastaafu, makomandoo au waliofukuzwa kazi ili ashirikiane nao kuwazuru viongozi akiwamo Sabaya.

Boaz anadai alimwambia Luteni usijitoe aendelee kumtafutia watu, alimtafutia watu wawili, mpango wa kumdhuru Sabaya ulikamilika, watuhumiwa walikamatwa mkoani Kilimanjaro, alifanya upelelezi kubaini uhusika wa Mbowe wakabaini kwamba yeye ndiye kinara.

Luteni Urio katika ushahidi wake anadai anaishi Morogoro Kihonda, Ofisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania kikosi 92 KJ, mstaafu na alimfahamu Mbowe, walikutana Mikocheni mwaka 2012, alimweleza harakati za ukombozi wa nchi.

Siku nyingine Mbowe alimpigia simu alitaka wakutane akasema hana nafasi, Mbowe alikataa kuzungumza kwa simu kutokana na aina ya mazungumzo.

Julai mwaka 2020 walikutana maeneo ya Mikocheni, Mbowe akamwambia kwamba CHADEMA kitachukua dola, Luteni Urio atapewa nafasi ya juu hivyo amtafutie mwanajeshi waliofukuzwa kazi, makomandoo na wastaafu ili wamsaidie katika harakati za kuchukua Dola.

"Niliamua kumpigia DCI Boaz nilimsimulia kwa sababu mimi ni mlinzi wa nchi yangu, Boaz akaniambia kila hatua watakayokuwa wanaifanya kina Mbowe niwe natoa taarifa.

"Mbowe alinitumia Sh. 500,000 kwa simu yake nikatoa Sh. 300,000 nikampa Halfani Bwire ikabaki simu Sh. 195,000, akatuma tena Sh. 199,000.

"Baada ya hapo Mbowe akakata mawasiliano na mimi, nikaamua kuwasiliana na Bwire kujua kinachoendelea," anadai katika ushahidi wake.

Anadai Bwire alimfahamisha kuwa wanatakiwa kumdhuru Sabaya kabla ya Agosti 7, 2020, walikuwa wanatumia mawasiliano ya telegrams kwa madai ndio salama.

Baadhi ya mashahidi wengine ni ASP Ramadhani Kingai, Mrakibu wa Polisi (SP) Jumanne, Inspekta Omari Mahita, Justine Kahaya alikuwa msaidizi wa Sabaya kabla ya kuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai.

Upande wa utetezi unadai miongoni mwa mashahidi wao ni Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai Lengai Ole Sabaya.



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akiteremka kwenye gari la Magereza wakati akiwasili Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# Kesi ya kikatiba ya Mbowe leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam leo inatarajia kuanza kusikiliza shauri la kikatiba lililofunguliwa na Mwenyekiti wa CHADEMa, Freeman Mbowe kupitia Wakili Peter Kibatala kupinga ukiukwaji wa haki zake za kikatiba.

Shauri hilo linasikilizwa mbele ya jopo la majaji watatu, Jaji John Mgeta, Steven Magoiga na Jaji Leila Mgonya.

Mahakama imefikia hatua hiyo, baada ya kukamilika kwa utaratibu wa kuwasilisha hoja za maandishi kwa pande zote mbili ambapo

Wakili Kibatala aliwasilisha kiapo cha nyongeza ili kuweka nyongeza ya mambo mbalimbali hadi kufikia Agosti 15, mwaka huu.

Jopo hilo liliamuru upande wa Jamhuri kujibu kiapo kinzani ndani ya siku 14 na Mahakama ilipanga tarehe ya kuanza kusikiliza Leo.

Wakili Peter Kibatala aliomba mahakama itoe hati ya kumleta Mbowe kila kesi hiyo inaposikilizwa, Mahakama ilikubali ombi hilo na kutoa hati, mshtakiwa huyo kuletwa leo.

Upande wa mlalamikaji unawakilishwa na Kibatala, Wakili John Mallya na Frederick Kihwelo huku Jamhuri ikiwakilishwa na Wakili Pius Hillar, Christopher Msigwa na Wakili Hang Changa.

Agosti 2, mwaka huu, Mbowe kupitia Wakili wake, Peter Kibatala aliwasilisha maombi Mahakama Kuu akitaka itamke kwamba kuna ukiukwaji wa haki zake za kikatiba katika kesi ya ugaidi inayomkabili.

Mbowe kafungua maombi dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali akidai wamevunja haki zake kikatiba kwa kushindwa kumpa nafasi ya kusikilizwa kikamilifu.

Katika maombi yake analalamikia kuvunjwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu Uchumi ambayo ameshtakiwa nayo kwa makosa ya ugaidi.

Wakili Kibatala anadai kwa mujibu wa sheria hizo mtuhumiwa anataka asishikiliwe zaidi ya saa 48 kituo cha polisi na akifikishwa mahakamani hakimu anatakiwa kuhakikisha kaelewa mashtaka yanayomkabili.

Anadai Mbowe kashikiliwa Oystebay tangu Julai 21, mwaka huu hadi Julai 26, alipofikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kushtakiwa kwa ugaidi.

Katika maombi hayo anadai sheria zimevunjwa, mteja wake alikaa kituoni zaidi ya saa 48, alilazwa sakafuni bila kujali usalama wa afya yake, wamevunja haki zake za kikatiba, wamemtesa na kumdhalilisha.

Polisi wanadaiwa kuvunja haki hizo kwa kushindwa kumpa nafasi ya kumsikiliza kikamilifu, walishindwa kutoa taarifa kwa mawakili wake ama ndugu yake wa karibu.

Anadai Mbowe alipelekwa mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba bila kuambiwa anakwenda wapi na alipopanda kizimbani mahakama ilikiuka haki za kikatiba kwa kushindwa kumuuliza kama kaelewa mashtaka yanayomkabili.

"Alitakiwa afahamishwe mashtaka yake kiufasaha, mashtaka mazito, mahakama haijamuuliza kaelewa ama la zaidi ya kumwambia haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo," alidai Kibatala katika maombi yake.

Anadai Mbowe hakupewa hati ya mashtaka hadi Julai 27, mwaka huu mawakili wake walipokwenda nayo gerezani.

"Tunaomba mahakama itamke kuna upungufu na haki za Mbowe zimekiukwa," alidai Kibatala.

## Samia aifagilia NMB huduma za kijamii

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan ameeleza kuvutiwa na kasi ya Benki ya NMB, baada ya kuongeza misaada ya kijamii katika kuadhimisha sherehe za kitamaduni za Kizimkazi visiwani Zanzibar.

Akizungumza wakati wa kilele cha Tamasha la Kizimkazi ambalo awali lilifahamika kama Kizimkazi Day, Rais Samia alisema NMB wamekuwa washirika wazuri tangu kuanzishwa kwa sherehe hizo mwaka 2016, wamekuwa naye bega kwa bega, huku wakiongeza misaada kila mwaka.

"Niwashukuru NMB kwa mchango mkubwa wanautoa kwenye sherehe hizi, kila mwaka tunao. Miradi mbalimbali katika sekta ya afya na elimu imefanyika," alisema Rais Samia.

Alibainisha kuwa tamasha hilo lilipoanza hakujua kama litakuwa kubwa namna hii, ambapo alisema historia yake ilikuwa ni kitendo cha wananchi wa Jimbo la Makunduchi kumfanyia sherehe ya kumuaga baada ya kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi mkuu wa urais mwaka 2015.

"Labda niwaambie malengo manne ya tamasha hili; lengo la kwanza ni kuwaleta pamoja wana Kizimkazi, kujuana na kupendana. Pili ni kulinda na kudumisha mila na desturi zetu, tatu kuhamasisha shughuli za maendeleo kupitia utekelezwaji miradi mbalimbali na nne ni kutangaza fursa za kiuchumi zilizopo eneo hili ikiwamo mambo ya kihistoria, fukwe za bahari na utalii wa kiutamaduni," alisema Rais Samia na kusisitiza kuwa:

"Lilipoanzishwa Tamasha la Kizimkazi mwaka 2016 liliitwa Samia Day, mwaka 2018 likabadilika na kuwa Kizimkazi Day, mwaka huu 2021 linaitwa Tamasha la Kizimkazi, utaona kila mwaka tunabadilika labda litakuja kuwa tamasha la wana Kusini wote."

Kwa upande wake Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara NMB, Filbert Mponzi, akizungumza kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema benki hiyo imefanya mambo makubwa visiwani Zanzibar hasa kwa kufuata kaulimbiu ya uchumi wa buluu kwa kuwaangalia wakulima wa mwani, wavunaji chumvi na wavuvi.

"Tumetoa mafunzo kwa wakulima wa mwani zaidi ya 3,400 juu ya masuala ya kifedha,pia tumewagusa wavunaji chumvi na wavuvi. Tumefanya haya kwa kuzingatia fursa zilizopo Zanzibar.

"Hadi sasa kwa Zanzibar katika sekta ya elimu na afya tumetumia zaidi ya shilingi milioni 257 tangu Agosti mwaka jana, jumla shilingi milioni 54 imetolewa kama misaada mwezi huu. Lakini katika kuadhimisha sherehe hizi za Tamasha la Kizimkazi kwa mwaka huu tumesaidia vifaa vya hospitali ikiwemo vitanda vya kujifungulia na mabati kwa ajili ya kuezekea baadhi ya shule, ambavyo kwa pamoja vina thamani ya zaidi ya shilingi milioni 35," alisema Mponzi.

Aidha, Mponzi alibainidha kuwa walipewa taarifa kuna Shule ya Msingi Ndijani ambayo aliwahi kusoma Rais Samia, kuna darasa limeangukiwa na mti, hivyo watahakikisha gharama zote za kulikarabati darasa hilo wanazitoa.

# Magomeni Kota wamlilia Samia kupigwa kalenda makazi mapya

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutoa neno kuhusu makazi hayo, wakidai ujenzi umekamilika na siku ya wao kuhamia zikisogezwa mbele kila uchao.

Wamesema hadi sasa baadhi ya wakazi hao wanaishi kwa ndugu, jamaa na wengine wakipanga na kwamba taarifa kuhusu kinachoendelea eneo hilo hazifikii.

Hata hivyo, jana Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliiambia Nipashe jana kwamba, suala hilo linasubiri uhakiki wa majina ya waliokuwa wakazi halali, hivyo wakazi hao wawe na subira.

Mwenyekiti wa wakazi wa Magomeni George Abel, akizungumza kwenye mkutano uliowakutanisha wakazi hao jana, mkoani Dar es Salaam, jirani na makazi hayo, alisema taarifa za hivi karibuni zilizoripotiwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari ni kati ya sababu mojawapo ya kuitisha mkutano huo.

Abel, alidai taarifa hizo zilieleza kwamba wakazi ambao watahamia kwenye kota hizo ni 300 pekee badala ya 644 ambao ndio walisajiliwa kabla ya ujenzi kuanza na kuhakikiwa Februari, mwaka huu.

"Hivi karibuni tulishangaa kusikia taarifa za aliyekabidhiwa ujenzi kusema wanaotakiwa kuhamia ni 300 tu, wakati sisi tupo 644, tulihakikiwa Februari 15 mwaka huu, na barua kama kamati kwenda kwa rais na waziri mkuu alikuja.

"Tunaomba rais asikie kilio chetu, tuliambiwa tutahamia Agosti lakini bado, wanasema hadi Oktoba mwaka huu ila kwa yanayoendelea tumeona tuyaseme," alisema Abel.

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo kwa takribani miaka 25, Salama Goronga, alisema kama mmoja wa zilizokuwa Kota za Magomeni, wanamwomba rais atoe neno kuhusu makazi hayo mapya ambayo bado wanasubiri siku ipangwe ya kuhamia.

"Hayati Magufuli alisema tuliokuwa wakazi tutakaa miaka mitano bila kulipa kodi, baadaye kuzinunua kwa bei nafuu, kwa sisi wakazi ambao tuliishi hapa na tukapisha ujenzi, leo hii waruhusiwe 300 pekee na sisi tuko zaidi ya 600 sio haki," alisema Salama.

**WAITARA**

Akielezea kuhusu suala hilo, Waitara alisema wakazi wa zilizokuwa Magomeni Kota wawe na subira wakati serikali ikifanya uhakiki wa majina ya wakazi halali, kabla ya kutangazwa siku rasmi ya wao kuhamia.

Kuhusu suala la wakazi hao kuishi bure kwa miaka mitano bila kulipa kodi, alisema litajadiliwa na serikali. "Majina yamepokelewa na yameenda kuhakikiwa na tuone nani aingie na nani asiingie, hayo majina yatatoka hadharani na kubandikwa na wahusika watashirikishwa. Wengine wanasema majina 300, wengine 600, wasubiri uhakiki wa serikali, wakiona maamuzi si sahihi, milango iko wazi.

"Majina yameandaliwa, serikali lazima ijiridhishe je anayeingia ni mwenyewe, mtu alikuwa mpangaji viwepo vielelezo nani alimpangisha. Ukisema nyumba kukaa bure miaka mitano nani atakataa, kila mtu atakuja," alisema Waitara.



Mkurugenzi wa Shule za St Mary's, Mutta Rwakatale, akimkabidhi cheti mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo wanaomaliza darasa la saba kwenye mahafali iliyofanyika shuleni hapo. Kulia ni Mkuu wa shule hiyo, Jacob Mwangi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukaguzi vyama vya siasa kuanza leo

**Na Elizabeth Zaya**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imesema inaanza leo kufanya ukaguzi kwa vyama vya siasa huku ikieleza kuwa ni takwa la kisheria kwa vyama vyote vyenye usajili kamili kuhakikisha vinakuwa na ofisi katika pande zote za Muungano.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Msajili, inaanza kuvikagua vyama hivyo pamoja na mambo mengine ni pamoja na kukagua ofisi za vyama hivyo Tanzania Bara na Visiwani.

"Uhakiki wa vyama vya siasa vyenye usajili kamili unatarajiwa kuanza kesho (leo), kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, kila chama chenye usajili kamili, kinatakiwa kuwa na ofisi pande zote mbili za Muungano," ilieleza taarifa iliyosainiwa na Naibu Msajili wa Ofisi hiyo, Sisty Nyahoza.

"Uhakiki huo utaanza na vyama vyenye ofisi zake Dar es Salaam na vyama vitakavyofungua kazi hiyo kesho (leo) ni AAFP na NRA. Jumanne uhakiki utaendelea kwa vyama vya UDP na NLD, vikifuatiwa na vyama vya UMD, na ADC Jumatano."

Alisema Alhamisi uhakiki huo utafanyika kwa vyama vya CCK, Demokrasia Makini na Ijumaa ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na UNDP.

Nyahoza alisema Septemba 6, ukaguzi utafanyika katika vyama vya NCCR-Mageuzi na CHAUMA na kufuatiwa na vyama vya ACT-Wazalendo, Chama cha Wananchi (CUF), TLP, SAU, ADA TADEA na DP.

Pia alisema uhakiki wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ukaguzi utafanyika kwenye makao makuu ya chama hicho jijini Dodoma, Septemba 10.

"Na baada ya kuhakiki vyama hivyo kwenye ofisi za Dar es Salaam, na Dodoma, zoezi litahamia ofisi za vyama hivyo Zanzibar kuanzia Septemba 13 kwa uhakiki vyama vya AAFP na NRA," ilisema taarifa ya Nyahoza.

Alisema uhakiki wa vyama vya siasa ni takwa la kisheria kuhakikisha vyama vyenye usajili kamili vinatekeleza masharti ya usajili kama yalivyoainishwa kwenye sheria ya vyama vya siasa na kanuni zake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Mafuriko Yanga kwa Mkapa yasiishie Siku ya Mwananchi*

**MAELFU** ya mashabiki na wanachama wa Yanga pamoja na wadau wa soka kwa ujumla, jana walijitokeza kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa katika tamasha la Kilele cha Siku ya Mwananchi.

Klabu ya Yanga ilitumia siku hiyo kutambulisha wachezaji wake kuelekea msimu mpya wa 2021/22, pamoja na kuuza vifaa mbalimbali vya klabu hiyo zikiwamo jezi, lakini mashabiki wa soka walipata burudani ya muziki kutoka kwa wasanii mbalimbali wakiongozwa na Koffi Olomide kutoka DR Congo.

Mbali na burudani na utambulisho huo, mashabiki wa soka pia walishuhudia mechi za timu zote tatu za klabu hiyo, kuanzia ile ya vijana wanawake (Yanga Princess) hadi ya wakubwa kwa upande ya wanaume ambayo ilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Zanaco ya Zambia.

Hakika ilikuwa zaidi ya burudani kwa wanachama, mashabiki na wadau wa soka kwa ujumla, ambao walihudhuria tamasha hilo lililokuwa la kuvutia zaidi ukilinganisha na misimu mingine ambayo klabu hiyo iliadhimisha Siku ya Mwananchi.

Hata hivyo, kwa maelfu yale ya mashabiki wa Yanga waliojitokeza, tunaona kuna jambo linahitajika kwa uongozi wa klabu hiyo kutazama ni wapi wanapokosea katika kuwahamasisha kuendelea kuhudhuria kwa wingi uwanjani kila timu yao inapocheza.

Kinachoonekana ni kwamba kuna uwezekano mkubwa mbali na mechi ama utambulisho wa wachezaji, huenda uwapo wa burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali, ulichangia kwa kiasi kikubwa kuwavutia mashabiki wa rika zote wanawake kwa wanaume kuhudhuria tamasha hilo.

Hivyo, uongozi wa Yanga lakini pia na klabu zingine, kuna haja ya kutazama namna nyingine ya kuwavutia mashabiki wa soka wa jinsia zote kwenda uwanjani ili kutunisha vipato vyao hasa ukizingatia udhamini unaotolewa kwa baadhi ya klabu bado haukidhi katika kujiendesha.


Kwa namna tamasha hilo lilivyofana kwa kuhudhuriwa na mashabiki wengi, ni wazi ipo haja sasa klabu za soka nchini kujaribu kujumuisha baadhi ya wasanii kutoa burudani kabla ya mechi pengine kutachangia kuvutia mashabiki wa jinsia zote kuhudhuria kwa wingi viwanjani na kuzifanya siku za mechi hususan za mwishoni mwa wiki kuwa sehemu ya 'mtoko' kwa familia mbalimbali.

Tunaamini endapo katika mechi za Yanga zitaendelea kuwa na angalau robo tatu ama nusu ya mashabiki kama waliojitokeza jana Uwanja wa Benjamin Mkapa, klabu hiyo inaweza kujiendesha kisasa kabisa kwa mapato ya mlangoni na kufanya makubwa zaidi kitaifa na kimataifa.

Tunatamani kuona hamasa ya mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani ikiendelea si tu kwa Yanga, bali kwa klabu zote, kwani kwa kufanya hivyo kutalingaza soka letu na hata kuvutia wachezaji wengi bora zaidi kutoka nje ya nchi kuja kucheza nchini, lakini wawekezaji wakubwa.

Ikumbukwe pia Yanga inaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikitarajiwa kutupa karata yake ya kwanza kati ya Septemba 10 -12, mwaka huu dhidi ya Rivers United ya Nigeria katika uwanja huo kabla ya kurudiana ugenini wiki mbili baadaye, hivyo matarajio yetu ni kuona idadi kama hiyo ikijitokeza ili kuipa sapoti timu yao na hatimaye kupata ushindi wa kishindo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# *Maandalizi ya ligi yawe bora kuepuka lawama*

Na Adam Fungamwango

**BAADHI** ya viongozi wa klabu za Ligi Kuu kwa sasa wapo kwenye hekaheka za usajili. Ikumbukwe kuwa ni kesho tu dirisha la usajili linafungwa. Kuna baadhi ya klabu zilishakamilisha usajili na sasa viongozi wao wako kwenye mikakati ya kuandaa timu zao kwenye mazoezi ya kwanza ya msimu, maarufu kama 'pre-season.'

Ni mazoezi ambayo wachezaji huyafanya wakiwa wametoka majumbani mwao baada ya mapumziko ya takriban mwezi mmoja hivi. Baadhi ya wachezaji hurejea wakiwa wamenenepa, lakini wengine wakiota vitambi pia. Kwa sababu tu walikaa majumbani wakifanya shughuli zingine na kukaa na familia bila kufanya mazoezi yoyote. Kifupi ni kipindi ambacho mchezaji anatakiwa kupumzika ili kuurudisha mwili wake kwenye hali yake ya asili.

Wanaporejea, wachezaji wengi wanakuwa hawapo kwenye shepu ile inayotakiwa ya kiuchezaji. Na pia wanakuwa hawana pumzi kama wanayotakiwa kuwa nayo wakiwa uwanjani.

Huu ndio wakati makocha wa viungo na pumzi wanapofanya kazi yao. Huwafanyisha mazoezi magumu, lengo likiwa ni 'kuwakamua', ili kupunguza mafuta waliyonayo na kuwa kwenye shepu ambayo mchezaji anatakiwa kuwa nayo.

Pia huongezewa pumzi, mazoezi haya hufanywa wakati mwingine takriban wiki mbili, kabla ya kuanza yale ya ufundi uwanjani. Kwa kawaida mazoezi haya ni muhimu zaidi kwani kama yakikosewa ni kwamba mchezaji hawezi kuwa fiti kwa msimu mzima.

Ni kwa sababu anakuwa hana tena muda wa kutengeneza stamina na pumzi wakati timu ipo kwenye ligi. Inakuwa ni kazi ya kusafiri, kucheza, kufanya mazoezi ya kiufundi tu kulingana na mpinzani unayecheza naye. Binafsi, natoa angalizo kwa viongozi wa klabu na makocha wao kuwa makini na kukitumia kipindi hiki vizuri. Kwa namna yoyote ile, kama wachezaji wao hawatofanyishwa vizuri mazoezi kipindi hiki, isitegemewe kama timu hiyo itafanya vizuri kwenye Ligi Kuu na michuano mingine yoyote ile.

Hii ni kwa sababu wachezaji watakosa stamina ya kuweza kuhimili dakika 90 au zaidi, mikikimikiki ya uwanjani, lakini watachoka mapema.

Tuliona baadhi ya timu kubwa tu msimu uliopita, ikifika dakika ya 65 mpaka 70, wachezaji wao wanakuwa hoi kutokana na kuchoka. Kuna baadhi ya watu huwa wanalalamika, au kuuliza sababu ya wachezaji kuchoka na kuhoji kama wanafanyishwa mazoezi.

Huwezi kumfanyika mchezaji mazoezi magumu ya stamina na pumzi wakati ligi inaendelea. Ni kumuumiza. Ukiona mchezaji anachoka mapema, au timu ni kwamba hawakukitumia vema kipindi hiki cha 'pre-season.'

Huwa kuna mazoezi tu ya kuweka mwili fiti, lakini kila kitu kinatakiwa kifanyike mwanzoni mwa msimu. Hiki ndicho kipindi chenyewe cha mazoezi magumu na pumzi na wala si kipindi cha masihara. Timu yoyote itakayokosea hapa basi itakuwa 'imekula' kwake.

Ndiyo maana nimeona niwakumbushe viongozi wa klabu, ili kutengeneza kambi nzuri, ni lazima kumulika paliko na miundombinu mizuri kwa mazoezi ya stamina, lakini pia chakula kizuri kwa wachezaji ambao wanafanya mazoezi ya aina hiyo, ili baaadaye wawaletee matokeo chanya.

Ninachoshangaa ni kwamba wakati baadhi ya timu zimeanza mazozi, zingine hata kocha hazina. Baadhi ndiyo kwanza zinaajiri makocha kipindi hiki. Zingine hadi dakika za mwisho bado zinapigana kwenye kusajili wachezaji.

Mshangao ni kwamba wachezaji hao watajiunga na timu hizo wakati gani, mazoezi yatakuwa ya muda gani hadi wawe fiti. Nasema hivi kwa sababu viongozi hawa hawa wanaojichelewesha, halafu timu zao zikifanya vibaya, lawama zinapelekwa kwa waamuzi, Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Bodi ya Ligi (TPLB).

Sina maana kuwa nawatetea waamuzi, la hasha. Ni kweli baadhi wamekuwa na matatizo, lakini mara nyingi kutokana na hilo, wamekuwa wakitupiwa pia zigo la lawama lisilo lao.

Timu inafungwa au haifanyi vizuri kwa sababu haikupata 'pre-season' nzuri, kisingizio kinakuwa ni waamuzi. TFF na Bodi ya Ligi.

Kuepuka hili, huu ndiyo wakati mzuri kwa viongozi wa klabu kuwa karibu zaidi na makocha na wachezaji, kuwapa kila wanachokipata kwa ajili ya maandalizi na si kusubiri timu zinaanze kusafiri huku na huko kwenda kucheza ligi ndiyo na wao wanazurura na kujifanya kuwa karibu na timu, wakati tayari wameshakosea huko nyuma. Matokeo yake kila mechi inapoisha inakuwa ni lawama tu.

# M'biashara mbaroni tuhuma kutorosha wanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

HATIMAYE Jeshi la Polisi limemkamata mfanyabiashara wa mjini Kyela, Bush Mwalusako, aliyekuwa akisakwa kwa zaidi ya miezi minane kwa tuhuma za kutorosha wanafunzi wawili wa kidato cha pili wilayani Kyela, mkoani Mbeya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Jumatatu iliyopita katika mpaka wa Namanga mkoani Kilimanjaro akiwa na mwanafunzi mmoja (jina lihifadhiwa) ambaye ni kati ya wawili waliokuwa wametoroshwa.

"Tumemkamata akiwa na binti (mwanafunzi) ambaye tumempeleka akapimwe na madaktari kujua kama alibakwa na mtuhumiwa amesharudishwa Mbeya kutoka mkoani Kilimanjaro," alisema.

Kamanda Matei alisema uchunguzi wa polisi utakapokamilika jalada litapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakayetoa uamuzi.

Taarifa kutoka wilayani Kyela na kuthibitishwa na kiongozi wa serikali ya kijiji, mwanafunzi mwingine kati ya hao waliokuwa wametoroshwa alirejea nyumbani kwao peke yake.

Wanafunzi hao walitoroshwa kwa nyakati tofauti tangu mwezi Januari, mwaka huu hali iliyosababisha sintofahamu kwa familia zao kwa kuwa walikuwa hawajui kama wapo hai.

Taarifa za kutoroshwa kwa wanafunzi hao ziliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kyela Mjini na kupewa RB namba KY41/RB/07/2021 na katika Kituo cha Polisi Kasumulu ISK/RB/41/2021.

Kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo kumechochewa na ufuatiliaji wa karibu uliokuwa ukifanywa na maofisa wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na taarifa zilizokuwa zikitolewa mara kwa mara kwenye gazeti hili.

Mei 16, 2021 Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, alipofanya ziara katika Wilaya ya Kyela, kufuatilia sakata la wanafunzi hao, walihakikishiwa na Jeshi la Polisi kwamba mtuhumiwa huyo angekamatwa ndani ya muda fupi.

"Tunalishukru Jeshi la Polisi kwa kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo japo imechukua miezi mingi sana tangu mfanyabiashara huyo afanye tukio hilo, tuna imani haki itatendeka kwa wanafunzi hao ambao wamekosa masomo kwa zaidi miezi saba sasa," alisema.

Henga alisema LHRC itaendelea kufuatilia kwa karibu tukio hilo hadi mtuhumiwa huyo atakapofikishwa mahakamani ili sheria iweze kuchukua mkondo wake kwa kuwa matukio kama hayo yamekuwa yakitokea kwa wingi nchini na kuishia njiani.

Mmoja wa wazazi wa wanafunzi hao, Simon Mwasitu, alipotembelewa na maofisa wa LHRC alisema sakata la kutoroshwa kwa mwanawe amekata tamaa kuendelea kulifuatilia polisi kwasababu Jeshi la Polisi limeshindwa kumtia mbaroni mfanyabiashara huyo kwa muda mrefu.

Alisema suala hilo ameamua kulikabidhi mikononi mwa Mungu kwa kuwa hivi sasa limeanza kumletea matatizo kifamilia na pia kuishi maisha ya wasiwasi kutokana na wakati mwingine kufungiwa nje mlango wa nyumba yake na watu wasiojulikana bila kufahamu lengo la watu wanaofanya kitendo hicho.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati) pamoja na viongozi mbalimbali wakiitikia dua iliyoombwa baada ya sala ya kumwombea marehemu Semeni Khamis Vuai, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC). Mbele ni Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Shekhe Khalid Mfaume, akiongoza dua hiyo katika Masjid Jamii-Attqwa Dunga na maziko kufanyika katika Kijiji cha Tunguu Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: IKULU**

# TPDC yatakiwa kulinda eneo la uwekezaji lisivamiwe

**Na Said Hamdani, LINDI**

UONGOZI wa Shirika la Mafuta na Petroli (TPDC), umetakiwa kutekeleza agizo la Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kufanya usafi na kuweka alama kuonyesha mipaka inayotambulika kuepusha eneo la uwekezaji mradi wa gesi asilia (LNG), kutovamiwa kwa shughuli za kijamii.

Dk. Karman alitoa agizo hilo wakati anazungumza na viongozi wa Mkoa wa Lindi, wakiwamo watendaji wa shirika hilo alipotembelea kuona utekelezaji wa agizo lake alilotoa miezi miwili iliyopita.

Aliwaagiza watendaji wa TPDC kulifanyia usafi wa mazingira eneo la uwekezaji mradi wa ujenzi kiwanda cha kuchakata gesi asilia, Likong'o, Kata ya Mbanja, Manispaa ya Lindi, kuweka alama kuonyesha mipaka sahihi ili wananchi wasilivamie.

Akizungumza na viongozi wa mkoa huo na watendaji wa TPDC, eneo hilo la mradi, alisema limeshatwaliwa na serikali na likiachwa bila ya kufanyiwa usafi na kuweka mipaka inayoonekana kwa usahihi, litavamiwa.

"Maagizo yangu nimeyatoa miezi miwili iliyopita, lakini hadi leo nimefika hapa sijaona kazi ya utekelezaji wake nini tatizo?" Alihoji Dk. Kalemani.

Alisema mpango wa kujenga kiwanda cha kuchakata gesi asilia upo pale pale, ikizingatiwa serikali tayari imeshaweka gharama mbalimbali ikiwamo ulipaji fidia kwa wananchi wa eneo husika waliokuwa wanaendesha shughuli za maisha yao.

Dk. Kalemani alisema kilichobaki kwa sasa ni ukamilishaji wa majadiliano kati ya serikali na wawekezaji yanayotarajia kufikia mwisho, mwezi Oktoba mwaka huu, huku akiwasisitiza wakazi wa Likong'o na Masasi ya leo kutolitumia tena.

Amempa muda wa wiki moja Meneja wa Mradi wa LNG, Fedister Agrey, kukamilisha taratibu zote ikiwamo eneo hilo kulifanyia usafi na kuweka alama ya mipaka.

Akijitetea mbele ya waziri, meneja huyo alisema kazi ya usafishaji wa eneo hilo itaanza sasa kwa kuwa tayari mkandarasi wa kufanya kazi hiyo ameshapatikana, kinachoendelea ni ukamilishaji wa taratibu ndogo ndogo.

Kufuatia maelezo ya meneja huyo, Waziri Kalemani alimpa muda wa wiki moja kukamilisha taratibu zote na kumpeleka mkandarasi eneo la tukio kuanza kazi ya kulifanyia usafi.

## Madereva wa magari ya serikali waonywa

**Na Costantino Michael, TUDARCo**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limewataka madereva wa magari ya serikali kuzingatia matumizi sahihi na salama ya barabara ikiwa na kufuata sheria, michoro na ishara za barabarani ili kupunguza ajali.

Limewataka madereva hao kutambua kuwa wote wanaomiliki leseni wako kwenye kundi moja la kutii sheria na kanuni za usalama barabarani, hivyo wasijione wapo juu ya sheria.

Jeshi hilo limeonya kuwa ikitokea wamekamatwa wakiwa wamevunja sheria, wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria kama madereva wengine.

Mossi Ndozero, Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma Trafiki Makao Makuu, aliiambia Nipashe jana mkoani Dar es Salaam kuwa kumeibuka wimbi kubwa la matukio ya madereva wa magari ya serikali kuvunja sheria za usalama barabarani kwa makusudi wakifikiri kuwa wao hawaguswi.

Aliwaonya kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya atakayekamatwa akifanya makosa barabarani.

"Imehimizwa zaidi kwenye kifungu cha sheria usalama barabarani namba 104 kuwa dereva wa serikali hayupo juu ya sheria kwa kuwa anaendesha chombo cha serikali.

"Wanatakiwa kutii sheria zaidi kuliko madereva wengine kwa kuwa wanabeba dhamana ya serikali na wakati mwingine wanakuwa na viongozi wetu kwenye magari yao, hivyo lazima wakumbuke kuwa hata yeye ni mtaji kwa serikali kwa kuwa anasaidia kutekeleza majukumu ya serikali," alisema.

Ndozero alisema wanatambua kuwa sio madereva wote wa magari ya serikali hawafuati sheria za usalama barabarani kwa kuwa wapo wanaotambua umuhimu wa kutumia taaluma yao waliyoisomea darasani na kikubwa zaidi wameongezewa elimu ya kuendesha viongozi, hivyo hutumia nguzo zote tano za udereva wawapo barabarani.

"Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani bado tunaendelea na jitihada za kutekeleza majukumu yetu ikiwamo kufanya operesheni, usimamizi wa sheria na utoaji elimu.

"Tunatoa elimu kwa madereva hao wa magari ya serikali huko huko maeneo yao ya kazi, lengo ni kuwafikia moja kwa moja," alisema.

# ACT yamtaka IGP Sirro kujiuzulu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimemtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, kujiuzulu, kwa madai kwamba ametoa matamshi yasiyofaa kwa familia ya mtuhumiwa wa mauaji ya askari watatu wa Jeshi la Polisi yaliyotokea wiki iliyopita.

Kwa mujibu wa taarifa ya chama hicho iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana na Naibu Katibu Mkuu wa Habari, Uenezi na Mahusiano ya Umma jana, Janeth Rithe, matamshi yaliyotolewa na Sirro ni kielelezo cha kukosa weledi.

"Ni jambo la kusikitisha kwa mtu kama ngazi ya IGP, anashindwa kufahamu kuwa hulka ya jinai ni suala la mtu binafsi na wala si la uzawa wala familia ya mtu," alisema Rithe.

"IGP Sirro ajiuzulu. Ni dhahiri kuwa IGP Sirro hana sifa ya kuliongoza Jeshi la Polisi lenye weledi kwa karne ya 21, kazi imemshinda, kachoka, analiabisha na kulishushia hadhi Jeshi la Polisi na mamlaka yake ya uteuzi. Tunamtaka ajiuzulu, la sivyo mamlaka yake ya uteuzi imwajibishe."

Chama hicho kilisema kimesikitishwa na kauli hiyo ya IGP Sirro.

"Chama cha ACT-Wazalendo kimesikitishwa na kauli ya IGP Sirro kwa kukebehi na kuilaumu familia ya Hamza Mohammed, anayedaiwa kushambulia askari wa jeshi hilo na kuwaua, kuwa wamemzaa mtoto ambaye ameleta balaa kwa Watanzania," alisema Rithe.

"Kwa maneno yake mwenyewe, IGP Sirro amenukuliwa kusema kwamba 'hiyo familia ya Hamza inajisikiaje, fikiria wewe ungekuwa baba yake Hamza, mama yake, mdogo wake, ungejisikiaje, kuzaa kwako umetuletea balaa Watanzania, kwa hiyo wengine wasituzalie watoto kama Hamza."

ACT- Wazalendo kupitia taarifa yake hiyo kilisema, matamshi ya IGP Sirro si ya kiungwana na yanakwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri inayokataza adhabu za jumla na kutweza utu wa watu.

"Ikumbukwe kuwa Hamza ni mtu mzima mwenye umri wa zaidi ya miaka 18, hivyo anawajibika kwa matendo yake na si ya wazazi wake au ndugu zake," alisema Rithe.

"Kauli ya IGP Sirro na mwenendo wa muda mrefu wa Jeshi la Polisi unadhihirisha kuwa tuna udhaifu mkubwa kwenye jeshi letu. Tanzania bado hatujaunda Jeshi la Polisi la kupambana na uhalifu na badala yake tunaunda jeshi la kupambana na vurugu, kuna maksi kubwa ya weledi kuanzia kwenye kuzuia uhalifu, uchunguzi na mahusiano ya kijamii baada ya uhalifu."

Pia, chama hicho, kilitaka kuundwa kwa tume huru ya kimahakama ya kuchunguza tukio la kushambuliwa na kuuawa kwa askari hao lililotokea Agosti 25, mwaka huu.

Katika tukio hilo watu watano walifariki dunia akiwamo kijana huyo Hamza, askari wa Jeshi la Polisi watatu na mmoja wa kampuni ya SGA.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akipokea zawadi ya picha kwa Mkurugenzi wa Shule za St Dominic Savio, Padri Aidan Ulungi, juzi wakati wa Jubilei ya miaka 25 ya mkurugenzi wa shule hizo mkoani Iringa. Kulia ni Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Iringa, Tarcisius Ngalalekumtwa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# TOL kutoa gesi ya oksijeni hospitalini

**Na Renatha Msungu**

KAMPUNI ya TOL Gas Limited imesema iko tayari kutoa mahitaji makubwa ya gesi ya oksijeni kwa ajili ya hospitali, baada ya kukamilika kwa ufungaji wa mtambo mpya wa kuzalisha gesi hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi wa Kampuni hiyo, Michael Shirima, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano mkuu wa wanahisa uliofanyika, jijini Dar es Salaam.

Shirima alisema mtambo mpya unatarajiwa pia kuongeza faida kwa kampuni yao tofauti na ule wa awali ambao ulikuwa unatengeneza hasara.

"Mtambo wa sasa utakuwa na faida kubwa kwa kampuni hivyo ni rahisi wao kuzalisha gesi hiyo," alisema Shirima.

Vilevile, alisema mwaka jana kulikuwa na changamoto nyingi na fursa pia zilikuwapo lakini changamoto hizo hazikuwa kwa TOL Gas pekee, bali duniani kote.

Hata hivyo, Shirima alisema kwa kipindi chote kampuni yao imethibitisha kuwa ni thabiti na inayoendana na hali halisi na imeendelea kuwa tayari kuendana na mahitaji ya mazingira ya soko lake.

Aidha, alisema utendaji kwa mwaka wa fedha 2020 uliongezeka kidogo

ikilinganishwa na mwaka 2019.

Kutokana na ukuaji wa mauzo hayo na faida iliyopatikana, alisema kampuni imetoa malipo ya gawio ya Sh. 34.78 kwa kila hisa ikiwa ni maradufu ya Sh. 17.37 zilizolipwa mwaka jana.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu, Daniel Warungu, alisema kampuni hiyo inamalizia ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha gesi ya kaboni wilayani Rungwe, mkoani Mbeya ili kufikia mahitaji makubwa ya ndani na nje ya gesi hiyo nchi za Zimbabwe, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Alisema bodi imejitosa kuwekeza katika usafirishaji wa gesi hiyo kuendana na uzalisha mpya.

Mauzo kwa mwaka huo yakikuwa kwa asilimia 15 kutoka Sh. bilioni 17.2 zilizopatikana mwaka 2019 mpaka Sh. bilioni 19.8.

Aliongeza kuwa faida kabla ya kodi ilikuwa kutoka Sh. bilioni 2.2 kwa mwaka 2019 mpaka Sh. bilioni 2.3 kwa mwaka wa fedha 2020.

# Ubovu barabara unavyohatarisha wagonjwa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga wamelalamikia kuwapo miundombinu mibovu ya barabara wilayani humo ambayo inasababisha wagonjwa kupoteza maisha wakiwa njiani kuelekea kwenye vituo vya huduma wakiwamo wajawazito.

Walisema hali hiyo hujitokeza hususani kipindi cha msimu wa mvua na barabara hizo hazipitiki na kuhatarisha maisha ya wagonjwa.

Walibainisha hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, na kuomba serikali kutengeneza miundombinu hiyo.

Diwani wa Mwataga, Matungwa Daudi, alisema wananchi wilayani humo wanapata shida wanapougua kwa kukosa usafiri wa uhakika kuwahi kwenye matibabu kutokana na ubovu wa barabara.

Alisema kutokana na ubovu wa barabara wananchi wanalazimika kutumia mikokoteni ya kukokotwa na ng'ombe.

"Tunaiomba serikali itujengee miundombinu ya barabara, ili kipindi cha msimu wa mvua ziweze kupitika na kuna mama mmoja alipoteza maisha kutokana na ubovu wa barabara, sababu alichelewa kufika hospitali kupatiwa matibabu," alisema Daudi.

Naye Diwani wa Mwakipoya, Thabisa Sadiki, alisema shida zingine katika wilaya hiyo ni uhaba wa watumishi wa afya.

Akizungumzia ubovu wa barabara, Meneja Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Kishapu, Samson Pamphili, alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021-2022 wametenga Sh. bilioni 2.4 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo ya barabara.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Dk. Shana Mdamu, alikiri kuwapo uhaba wa watumishi wa afya.

Alisema mahitaji ni watumishi 487, lakini waliopo ni 283, upungufu 204, zahanati 44, vituo vya afya saba na hospitali moja ya wilaya na kwamba wameomba kupatiwa watumishi wengine.

**"Tunaiomba serikali itujengee miundombinu ya barabara, ili kipindi cha msimu wa mvua ziweze kupitika na kuna mama mmoja alipoteza maisha kutokana na ubovu wa barabara, sababu alichelewa kufika hospitali kupatiwa matibabu," alisema Daudi.**

HABARI KITAIFA

## Rwakatale ataka maadili mema kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI na walezi wamehimizwa kufuatilia mienendo ya watoto wao na kuwalea kwa misingi ya maadili mema na kuwapatia elimu bora itakayowasaidia kujitegemea wanapokuwa wakubwa.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Shule za St. Mary's Mutta Rwakatale, kwenye mahafali ya kuwaaga wanafunzi wa darasa la saba katika shule hiyo yaliyofanyika kwenye Shule ya St Mary's Mbagala mkoani Dar es Salaam.

Alisema kila mzazi anajukumu la kuhakikisha kuwa anamwelimisha mwanawe kwa hali yoyote ile ili atakapokuwa aweze kumsaidia na kusisitiza kuwa watoto wanahaki ya kusikilizwa katika mahitaji yanayowasaidia kutimiza malengo yao.

"Mtoto anapokuomba umpeleke kwenye masomo ya ziara wakati wa likizo, umnunulie daftari, kalamu na vitu vingine vinavyomsaidia katika masomo yake jitahidi umpatie kwani mafanikio yake ni furaha kwetu sisi walimu kwenu wazazi na kwake pia, watoto ndio viongozi, madaktari, marubani walinzi na nguvukazi ya taifa kwa baadaye tuwalinde na kuwarithisha elimu bora.

Tuwe na tabia ya kuwajenga watoto watu kiimani tukifanya hivyo watakuwa na hofu, wengine ni wakorofi lakini tukiwa na kawaida ya kuongea nao kwa kuwaelekeza taratibu watakuelewa," alisisitiza.

Aliwataka wazazi pia kuwasisitiza wanafunzi hasa wa darasa la saba wanaotarajia kufanya mtihani wa kuhitimu wiki mbili zijazo kuhakikisha kwamba wanasoma kwa bidii ili watimize malengo yao.

Aidha, watoto wanategemewa na familia na taifa kwa ujumla hivyo wanapaswa kujilinda na kuwa na tahadhari wasijihusishe na makundi mabaya mitaani wanaporudi nyumbani kwa ajili ya mapumziko mafupi.

"Mnapomaliza mitihani na kurudi nyumbani kunawatu wengi watawatazama na wengine wanaweza kujaribu kuwashawishi ili mjiunge nao hakikisheni mnawaepuka kwani watasababisha mshindwe kutimiza malengo yenu," alisema.

"Simamieni na myaendeleze maadili mliyopatiwa na wazazi pamoja na walimu wenu hapa shuleni bado mnasafari ndefu ya kimasomo msije mkabweteka," alisema.

Aliwataka kutumia elimu waliyoipata kupambana na changamoto za maisha kwani kunachangamoto nyingi na aliwataka wasikubali kukatishwa tamaa na wakashindwa kutimiza malengo yao.

# Wazazi lawamani kuhamisha watoto kukwepa ulipaji ada

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa baadhi ya wazazi sio waaminifu wanapojua wamelimbikiza madeni ya ada, katika shule, hivyo kushindwa kulipa na baadaye kuwahamishia watoto wao shule zingine bila kufuata utaratibu.

Imebainishwa kuwa kutolipwa kwa madeni hayo kunachangia kurudisha nyuma mapato ya shule.

Hayo yalisemwa na Bahati Dickison, Mwalimu Mkuu wa Shule ya awali na msingi Ebonite, wakati wa mahafali ya wahitimu wa elimu ya awali na msingi.

"Shule yetu inatoa elimu bora, lakini baadhi ya wazazi wameshindwa kulipa madeni ya ada, wamewahamisha watoto wao bila kufuata taratibu za uhamisho," alisema.

Mwalimu Bahati alisema kuwa shule yao ina maktaba ambayo imekuwa ni mkombozi kwa wanafunzi kwa kuwa inawasaidia wanafunzi kujifunza kusoma na kuandika.

Alisema kutokana na shule yao kutoa elimu bora ikiwamo na kufanya vizuri katika mitihani ya taifa kila mwaka, idadi ya wanafunzi imezidi kuongezeka katika shule hiyo.

Alisema shule yao pamoja na kuwa inatoa elimu ya awali na msingi pia ina Chuo cha Ualimu ambapo na kozi za elimu maalumu inatolewa.

Mwalimu huyo aliwataka wazazi kuwa na mipaka katika masuala ya teknolojia ili kuwanusuru watoto wao.

Akizungumza masuala ya Covid-19, alisema kuwa katika kujilinda wanafuata taratibu za kiafya ikiwamo na kuchukua tahadhari ambapo kila mwanafunzi analala katika kitanda chake peke yake.

Ofisa Elimu Taaluma, Manispaa ya Ubungo, Abdallah Buheti, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo alikiri kupokea malalamiko katika shule za binafsi juu ya wazazi kuwahamisha watoto bila kulipa madeni ya ada katika shule walizotoka.

"Taarifa nazipata za wazazi kuhamisha watoto bila kulipa ada, tatizo hilo kwa sasa halitajitokeza kwa kuwa tumetoa 'password' kwa walimu wakuu mtoto anapohamishwa taratibu zitafuatwa kati ya mwalimu mkuu wa shule atokayo mtoto na shule aendayo mtoto, hapo mzazi hawezi kukwepa ulipaji wa ada anayodaiwa," alisema.

Alisema uwapo wa shule binafsi ni faida kubwa kwa serikali kutokana na kujifunza vitu mbalimbali kupitia shule hizo, na kwamba hali hiyo imechangia shule za serikali kuboresha miundombinu yake, hivyo kuongeza ufaulu.

Pia alisema Shule ya Ebonite ni moja ya shule zinazofanya vizuri mitihani yake ya kitaifa katika Manispaa ya Ubungo.




Wakala wa kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania akimpa maelekezo mkazi wa Dar es Salaam juu ya kampeni mpya ya 'Kimbiza na 4G ya Ukweli' yenye lengo la kuifahamisha jamii kuhusu kasi na uhakika wa mtandao wake unaowezeshwa na uwekezaji katika teknolojia pamoja na upana wa huduma inazotoa kwa wateja wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yaipatia Zanzibar kliniki inayohamishika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amekabidhiwa kliniki inayohamishika iliyotolewa na Benki ya NBC kwa serikali ya Zanzibar.

Kliniki hiyo ilitolewa ili kuboresha huduma ya afya hususani ya mama na mtoto visiwani humo sambamba na kuzindua jengo la madarasa ya shule ya maandalizi ya Kizimkazi yaliyojengwa na kukarabatiwa kwa msaada wa benki hiyo.

Hafla ya uzinduzi na makabidhiano hayo ilifanyika katika Kijiji cha Kizimkazi Mkunguni Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar na kuhudhuriwa na baadhi ya viongozi waandamizi wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar, akiwamo Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto Zazibar, Ahmed Nassor Mazrui na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Haroun Ali Suleiman. Alikuwapo pia Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, viongozi wa Benki ya Taifa ya NBC na wakazi wa kijiji hicho.

Akizungumza wakati akizundua na kukagua jengo hilo pamoja na kliniki hiyo, Rais Samia aliishukuru benki hiyo kwa jitihada hizo, huku akitoa wito kwa taasisi hiyo pamoja na taasisi nyingine za kifedha kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

"Hongereni sana kwa jitihada hizi zinazowagusa wananchi moja kwa moja na zaidi naombeni sana mwendelee kuiunga mkono serikali katika kuwaleta maendeleo wananchi katika maeneo yote," alisema Rais Samia.

Awali akizungumza ofisini kwake wakati akipokea msaada wa vifaa tiba ikiwamo UtraSound mashine vinakavyotumika kwenye kliniki hiyo, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Ahmed Nassor Mazrui, pamoja na kuishukuru benki ya NBC kwa msaada huo, alisema serikali hiyo itahakikisha msaada huo unatumika kama ilivyokusudiwa.

"Msaada huu ni muhimu na unahitajika sana. Jukumu letu kama serikali ni kuhakikisha vifaa hivi vinatunzwa na vinatumika kama ilivyokusudiwa ili vilete tija iliyolengwa kwa maana visaidie haswa kuokoa maisha ya wazanzibar wakiwamo kinamama na watoto hasa walipo pembezoni.

Aliahidi kwa niaba ya serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendeleza ushirikiano na benki hiyo hususani kwenye masuala mbalimbali ikiwamo yale yanayohusu ustawi wa jamii huku akibainisha kuwa uimara wa benki hiyo kwenye utoaji wa huduma zake visiwani humo kwa kiasi kikubwa unachagizwa na namna inavyoshirikiana na jamii ya Wazanzibar ikiwamo kibiashara na mambo ya kijamii.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 275, ni muendelezo wa jitihada za benki hiyo za uwajibikaji kwa jamii zinazosukumwa na dhamira kuu ya taasisi hiyo katika kushirikiana na jamii inayoihudumia.

"Benki ya NBC tumekuwa tukiguswa na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye huduma za afya na elimu hapa nchini ikiwemo Zanzibar na ndio maana tumekuwa mstari wa mbele kuhakikisha tunashirikiana na serikali zote mbili kukabiliana na changamoto zinazohusu sekta hii muhimu." Alisema huku akibainisha kuwa benki hiyo inaendelea kufanya jitihada zaidi ili kufanikisha misaada kama hiyo kwenye maeneo mengine ikiwemo visiwani Pemba. Alisema huduma zitakazotolewa na kliniki hiyo kwa kinamama na watoto zitatolewa bure kwa kuwa zitagharamiwa na benki hiyo kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Pamoja na msaada huu benki ya NBC itaendelea kuhudumia vifaa vilivyopo ndani ya kliniki hii hata pale vitakapokuwa vinapata hitilafu za kiufundi. Tunaamini sasa kupitia huduma hii wataalamu wa afya wataweza kuwafikia walengwa popote walipo hususani wale waliopo pembezoni hususani wakina mama na watoto na kupitia msaada wa mwenyezi Mungu tutaweza kuokoa maisha yao," aliongeza.

Mbali na ujenzi wa jengo la Madarasa katika wa skuli ya maandalizi Kizimkazi msaada huo pia umehusisha samani za ndani ya madarasa hayo ikiwamo madawati na meza sambamba na jiko kwa ajili ya upishi wa chakula cha wanafunzi hao pamoja na vifaa vya michezo ili kutoa fursa ya watoto kufurahia michezo yao. Akizungumzia msaada huo wa kliniki inayohamishika, Mratibu wa Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto, Wizara ya Afya Zanzibar, Wanu Bakari, alisema msaada huo umefika wakati muafaka kwa kuwa serikali hiyo inapambana kusogeza huduma za afya hususani maeneo ya pembezoni ili kuepukana na changamoto ya vifo vya kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

"Tunaishukuru sana benki ya NBC kwa kuliona hili na kwa kweli wametugusa sana! Kwa mfano kupitia kliniki hii tutaweza kutoa huduma ya Utrasound ambayo ni muhimu sana. Kwa kwasasa tunakabiliwa na uhaba wa huduma hii hivyo kupitia msaada huu tatizo linakwenda kupungua."

# Mtuhumiwa wa udhalilishaji mtoto adai mgonjwa wa akili

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MTUHUMIWA Nassor Issa Nassor (30) mkazi wa Kizimbani Wete, amedai kuwa hana hakika kuwa alimwingilia mtoto wa kike (9) kinyume cha maumbile, kwa vile amekuwa akiugua ugonjwa wa wasiwasi mara kwa mara.

Alitoa madai hayo katika Mahakama ya Mkoa 'A' Wete Pemba, wakati akijitetea kutokana na tuhuma zinazomkabili, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake wiki mbili zilizopita.

Alidai kuwa kitu anachokikumbuka, polisi walikwenda nyumbani kwao na kumchukua bila kujua kosa alilofanya.

Alidai hakupinga kuwafuata, ingawa walianza kumpiga na ndipo aliwauliza na kujibiwa kuwa akifika kituo cha polisi ataambiwa kosa lake.

Alidai baada ya kufika aliambiwa alimdhalilisha kinyume cha maumbile mtoto wa miaka tisa, tuhuma ambazo alizikanusha.

"Mheshimiwa hakimu, mimi wananizulia tu, sijafanya kitu, lakini walikuja askari kunichukua nyumbani bila kujua kosa mpaka wakaniambia," alidai.

Alidai anapofanya jambo huwa hajijui kwani ni mgonjwa wa wasiwasi tangu alipokuwa mdogo na ameshapelekwa hospitali na wazazi wake.

Baba mzazi wa mtuhumiwa, Issa Nassor, alipoulizwa na Hakimu wa Mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, kuhusu ugonjwa wa mwanawe, alidai ni mgonjwa wa akili tangu alipokuwa akisoma darasa la saba.

"Aliacha kwenda skuli kwa ugonjwa huo darasa la saba na tushakwenda hospitali ya Wete, Chakechake, na Dar-es-Salaam lakini hatujafanikiwa," alidai baba huyo. Alidai wakati mwingine anakuwa vizuri kiakili, ingawa wakati mwingine anakuwa mgonjwa wa kupita majalalani na kuokota makopo.

Hata hivyo, baba huyo hakuwa na kielelezo chochote cha hospitali kuithibitishia mahakama kwamba, mwanawe huyo ni mlemavu wa akili.

"Mheshimiwa hakimu leo sina vielelezo hapa nimevisahau, lakini siku ya upelelezi vilihitajika na nilikwenda navyo vyote," alidai baba wa mtuhumiwa huyo.

Baada ya utetezi huo Hakimu Shamhun aliliahirisha shauri hilo hadi kesho kwa ajili ya kutolewa hukumu.

Awali ilidaiwa kuwa, mtuhumiwa huyo alitenda makosa mawili, ambapo kosa la kwanza alilitenda Julai 26 mwaka jana saa 1:30 za usiku katika Shehia ya Bopwe Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali na bila ya ridhaa ya walezi wake, alimtorosha mtoto huyo kutoka nyumbani kwao na kwenda nae migombani hapo hapo Bopwe, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Kosa la pili anadaiwa kulitenda siku hiyo hiyo, ambapo alimwingilia kinyume cha maumbile mtoto huyo.



Mtaalamu wa maabara kutoka Mpango wa Taifa wa Damu Salama Kanda ya Mashariki, Fimbo Emmanuel, akimtoa damu Murtadha Rashid mmoja wa waumini wa Juimuiya ya Khoja Shia Ithnasheri Jamaat (KSIJ), wakati wa kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha kiongozi wa dhehebu hilo, Imamu Hussein, kwenye msikiti wa KSIJ jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Asasi yaikosha serikali elimu kukabili umaskini, magonjwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mwanaid Ali Khamis, ameipongeza Asasi ya Ruvuma Orphans Association (ROA) kwa utoaji elimu juu ya masuala ya ustawi na maendeleo.

Asasi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa makundi yaliyopo katika hatari ya kuathirika au kuathiriwa na umaskini na magonjwa.

Akizungumza alipotembea Asasi ya Roa mjini hapa, Mwanaid Ali alisema kuwa serikali ina mipango mingi ambayo inapaswa kuungwa mkono na wadau wake wa maendeleo zikiwamo asasi za kiraia.

Alisema kuwa amefarijika sana kuona kuwa Asasi ya Roa imekuwa ikishiriki kikamilifu kutoa elimu ya kujingika na magonjwa na upatikanaji wa mimba za utotoni kwa vijana barehe wenye umri wa miaka 10-19 ambao ni asilimia 22.9 ya idadi ya Watanzania wote.

Alisema hili ni kundi kubwa ambalo serikali imewekeza nguvu kubwa za kuhakikisha wanalindwa dhidi ya changamoto zinazowakabili zikiwamo mimba za utotoni, magonjwa ya ngono na utumiaji wa dawa za kulevya.

"Nimefarijika sana kusikia kuwa shirika hili limekuwa likitoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwani jitihada hizo zinaunga mkono mpango mkakati wa taifa wa kutokomeza aina zote za ukatili kwa makundi hayo," alisema Mwanaid.

Awali Mwenyekiti wa ROA, Mathew Ngalimanayo, akitoa neno la utangulizi mbele ya Naibu Waziri Mwanaidi, alisema dhamira ya ROA ni kubuni, kupanga na kutekeleza mipango inayolenga kuwafikia, kuwasaidia, kuwaokoa na kuwaendeleza watu walio katika hatari ya kuathirika/kuathiriwa na umaskini na magonjwa kwa kushirikiana na wananchi, serikali na wadau wengine.

Ngalimanayo alisema katika utekelezaji wa mradi wa matunzo na kinga dhidi ya VVU/Ukimwi wamewafikia wasichana na wanawake wanaofanya biashara ya ngono 3,201 (Manispaa ya Songea 1,670, Wilaya ya Songea 0, Halmashauri ya Mji Mbinga TC 0, Halmashauri ya Wilaya Mbinga 568 na Halimashauri ya Wilaya ya Nyasa 963 kati ya lengo la kuwafikia walengwa 4,022 ambayo ni sawa na asilimia 80 ya lengo la mradi.

Pia wamewafikia wasichana wa rika balehe na wanawake wadogo 8,082 (Manispaa ya Songea 1319, Halmashauri ya Wilaya Songea 2,698, Halmashauri ya Mji Mbinga 2,078, Halmashauri ya Wilaya Mbinga 941 na Halmashauri ya Wilaya Nyasa 996 kati ya lengo la mradi la kuwafikia walengwa 9,846 ambayo ni sawa na asilimia 80. Alisema kuwa wamefanikiwa kuwafikia watu 31,191 kati ya hao watu 11,458 walipimwa VVU kupitia njia ya huduma ya mkoba watu 7,056 walipimwa kupitia njia ya ufuatiliaji wa mnyororo wa wateja na watu 12,677 walipimwa kupitia njia ya Jipime.

Alieleza zaidi kuwa wamefanikiwa kuwafikia watu 1,168 kati ya lengo la kuibua visa 771 waliopata changamoto za ukatili wa kijinsia na kuwapatia rufani kwenda maeneo ya kupata huduma husika. Hii ilikuwa ni sawa na asilimia 152, pia wamefanikiwa kuwafikia watu 2,531 na huduma ya Dawa Kinga kati ya lengo la watu 10,417.

Aidha, wamefanikiwa kuwaunganisha watu 1,609 wanaoishi na VVU/Ukimwi kwenye kliniki ya tiba na matunzo na huduma zingine.

## Waafikiana kuchangishana fedha za chakula shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZAZI wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Boko Timiza Kata ya Tumbi Halmashauri ya Mji Kibaha, wameridhia kuchangishana fedha kwa ajili ya chakula kwa watoto wawapo shuleni.

Katika kikao kilichofanyika mwishoni mwa wiki kilichoitishwa na Diwani wa Tumbi, Raymond Chokala, walikubaliana kila mzazi kuchangia Sh. 200 kwa siku ili mtoto aweze kupata chakula.

Diwani Chokala aliitisha kikao hicho baada ya maelekezo yaliyotolewa hivi karibuni na Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, akielekeza kila shule wanafunzi wapate chakula kuondoa udumavu.

Akizungumza baada ya kikao hicho, Chokala alisema amelazimika kufanya vikao kutokana na wazazi kwenye shule za msingi tano zilizopo katika kata hiyo kushauriana namna ya wanafunzi kupata chakula wakiwa shuleni.

Alisema kuwapo kwa chakula shuleni itaondoa udumavu ni njia mojawapo ya kuinua ufaulu kwa wanafunzi.

## TADB na PASS kuwazesha vijana

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imekubaliana kimkakati na kampuni binafsi inayojishughulisha na kilimo ya Private Agricultural Sector Support (PASS Trust) yanayolenga kuwewezesha vijana na wanawake kupata mikopo itakayoinua shughuli zao za kilimo hapa nchini.

Akizungumza muda mfupi, baada ya kufanya mazungumzo, Mkurugenzi Mtendaji wa PASS Trust, Johane Kaduma, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema makubaliano ya taasisi hizo mbili yanalenga kuwawezesha vijana na wanawake ili waweze kunufaika na mikopo moja kwa moja sambamba na kuchangia maendeleo ya ukuaji wa sekta ya kilimo.

"TADB na wenzetu wa PASS Trust wote tumekuwa tunajishughulisha na kuinua sekta ya kilimo, hivyo kutokana na umuhimu huo tumekubaliano kuongeza nguvu na hasa kwa vijana ambao ndio nguvu kazi kwa taifa na wanawake ambao sehemu kubwa wamekuwa wakijishughulisha na kilimo waweze kupata mikopo nafuu itakayo wanufaisha kuendesha shughuli za kilimo chenye tija," alisema Nyabundege.

Kwa upande wake, Kaduma aliishukuru na kuipongeza TADB kwa jitihada wanazozifanya katika kuleta mageuzi ya katika sekta ya kilimo na kueleza kuwa taasisi yake inajivunia kuingia ubia na benki hiyo ambayo itawafungulia fursa vijana kuweza kujiajiri kupitia mikopo.

"Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Kazi Duniani (ILO), ukosefu wa ajira unakadiriwa kuwa asilima 13.4 kwa vijana wenye umri wa miaka 15 mpaka 34, huku imani yangu ni kuona vijana hawa wakinufaika na ubia huu ili kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira nchini," alisema Kaduma.

Nipashe
# Spotika



LIGI 10 ZILIZOTUMIA FEDHA NYINGI USAJILI MSIMU 2021-22 UK. 12 - 13



# WACHEZAJI WATAKAOTESEKA KUTUA KWA RONALDO UNITED

## ISIKUPITE

ROBERT Lewandowski amefunga mara 13 mfululizo kwenye Bundesliga, akiifukuzia rekodi ya Gerd Muller aliyoiweka mwaka 1970 kwa kufunga mara 16 mfululizo. Nyota huyo wa kimataifa wa Poland alifikia hatua hiyo wakati akitupia hat-trick, Bayern Munich ikiichapa Hertha Berlin mabao 5-0 juzi, lakini pia alifikisha mabao 301 kwenye mechi 333 za ligi hiyo.



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ilitangaza Ijumaa usiku kuwa wamekubaliana na Juventus kuhusu kurudi kwa Cristiano Ronaldo na lilikuwa ni sakata fupi la uhamisho zaidi wakati wa majira haya ya joto. Man United waliteka nyara hatua ya Manchester City kwa Ronaldo na kuwasili kwake ni kitita cha keki katika dirisha nzuri la uhamisho wa msimu huu wa majira ya joto.

Man United walipaswa kusonga mbele na kumsajili kiungo wa mkabaji, lakini kuna nafasi nzuri sana kwamba, isingetokea kabla ya mwisho wa dirisha hili la uhamisho. Kwa hiyo, Ronaldo ni usajili mzuri.

Huku Edinson Cavani akiripotiwa kukosa mechi kadhaa kutokana na majukumu ya kitaifa, kuwa na Ronaldo kwenye kikosi ni jambo kubwa. Kuwa na 'masta' kama huyo kwenye vyumba vya kubadilishia nguo kutasaidia kuinua kiwango na kuiboresha timu nzima.

Athari ambayo Ronaldo atakuwa nayo kwa vijana wengine wa Man United inaweza kuwa kubwa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ataiboresha sana Man United na ni ngumu kupata kikosi hatari zaidi cha ushambuliaji kuliko kile cha Mashetani Wekundu hivi sasa.

Wakati kuwasili kwa Ronaldo ni habari njema kwa klabu na mashabiki, kuna watu wachache ambao wanaweza kuathiriwa vibaya na hilo.

Bila kuchelewesha zaidi, ngoja tuangalie wachezaji wanne ambao wanaweza kuteseka sana kutokana na kuwasili kwa Ronaldo, hawa hapa...

### #4. DANIEL JAMES

Daniel James labda ndiye mshambuliaji aliyeboreshwa zaidi kiufundi katika kikosi cha Man United hivi sasa. Lakini yeye ni mchezaji anayejituma katika mazoezi na ni mtu mwenye ustadi uwanjani.

James ni ishara ya mawazo ambayo kocha, Ole Gunnar Solskjaer anataka kuingiza kwa upande wake na ndio sababu raia huyo wa Wales ni sehemu ya timu. Wacha tukabiliane na hilo. James ni mchezaji wa kikosi. Isipokuwa kuna haja ya kuzunguka au kuwa na kazi maalum (kama vile kubabaisha walinzi nyuma na kasi yake kwa mfano) inahitaji kufanywa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 haanzi kwa Man United.

Kuwasili kwa Ronaldo hakika kumeboresha utajiri wa kushambulia wa 'Mashetani Wekundu' hao. Wana wachezaji kama Mason Greenwood, Marcus Rashford, Anthony Martial na Cavani ambao wanaweza kucheza mahali popote mbele.

Pia wana Jesse Lingard na Amad Diallo kwenye mishahara yao pia. Inatosha kusema, James ameanguka zaidi chini. Ana uwezekano mdogo mno wa kupata nafasi ya kucheza na hilo linaweza kudhoofisha maendeleo yake katika hatua muhimu kwenye maisha yake ya soka.

### #3. EDINSON CAVANI

Haikumchukua muda mrefu Edinson Cavani kuwa mtu anayeabudiwa kati ya waaminifu wa Old Trafford. Nyota huyo wa Uruguay alikuwa na ushawishi mkubwa kwa mashabiki wengi na uchezaji wake wa mbele katika msimu wa 2020-21. Alifunga mabao kadhaa muhimu kwa Man United.

Lakini kuwasili kwa Ronaldo, kunaweza kufanya Cavani kuonekana si muhimu kama sehemu ya timu. Upande wa mfumo wa Solskjaer haufanyi kazi na washambuliaji wawili. Kwa hiyo licha ya kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na klabu hiyo, Cavani ana uwezekano mdogo wa kuwa mshambuliaji mkuu wa Man United msimu huu.

Yeye ni mshambuliaji mzuri zaidi wa chaguo la pili, lakini haijulikani ni wapi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, atasimama kucheza jukumu kama hilo. Lakini matokeo yanayowezekana ni kwamba Ronaldo au Cavani watasumbuliwa na ukosefu wa wakati wa kucheza. Cavani ana uwezekano wa kuchukua anguko kuliko Ronaldo.

### #2. ANTHONY MARTIAL

Anthony Martial alikuwa mmoja wa wachezaji bora wa Man United msimu wa 2019-20. Alifunga mabao 23 na kutoa asisti 12 katika mechi 48 kwenye mashindano yote msimu huo. Solskjaer alikuwa amemfanya mshambuliaji mkuu na alijitahidi kadri awezavyo kulipa imani iliyoonyeshwa kwake na kocha wake.

Lakini hakuwa na wakati mzuri mwishoni mwa msimu, akifunga mabao tisa tu na kutoa usaidizi mara saba katika mechi 36 kwenye mashindano yote. Hii imekuwa hadithi ya Martial kukaa benchi pale United hadi sasa.

Hakuwa na nafasi chini ya Cavani na Greenwood kwa msimu uliopita na sasa kuwasili kwa Ronaldo kunaweza kuwa msumari wa mwisho kwenye jeneza la Martial.

Hatakuwa na uwezo pia wa kucheza katika nafasi anayopendelea kama mshambuliaji wa kati, kwani kuna wafungaji watatu waliothibitishwa kwenye kikosi hicho hivi sasa.

Atahitaji kushinda au kuwa na kiwango cha juu zaidi ya wachezaji kama Jadon Sancho, Marcus Rashford na Greenwood ili aweze kupata nafasi ya kuanza kwenye kikosi cha Man United.

### #1. BRUNO FERNANDES

Bruno Fernandes amefanikiwa sana akicheza kama mshambuliaji wa pili au namba tisa wa uwongo. Amechukua nafasi ya juu uwanjani.

Shida ni kwamba, Ronaldo anapenda kushuka chini na kufanya kazi katika maeneo ambayo Fernandes anacheza. Ushawishi wa Fernandes unaweza kupungua wakati yeye si 'hirizi' ya timu. Hii pia hufanyika wakati wakiwa kwenye timu ya Taifa ya Ureno, ambapo timu hiyo imejengwa kumzunguka Ronaldo.

Fernandes amehusika kidogo katika kufunga mabao kwa Ureno. Ikiwa kuna mabadiliko kama hayo pale Man United, umuhimu na mchango wa Fernandes unaweza kupungua sana.

Extra Time

# LIGI 10 ZILIZOTUMIA FEDHA NYINGI USAJILI MSIMU 2021-22



ROMELU LUKAKU

**LONDON,** England

ZAIDI ya mwaka baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, matatizo ya kifedha bado yanaendelea kuikumba dunia, hasa kwenye soka.

**Mlipuko huo ulifanya klabu nyingi kubwa kuyumba kwa kiasi kikubwa mno na miongoni mwao ni miamba ya soka la Hispania, Real Madrid na Barcelona. Klabu hizo mbili zipo kwenye wakati mgumu na hivyo kushindwa hata kufanya usajili wa maana kipindi hiki cha majira ya joto.**

Hata hivyo, bado kumekuwa na usajili wa fedha kubwa kipindi hiki cha majira ya joto.

Jack Grealish amehamia Manchester City kwa euro milioni 117.5, huku Chelsea wakitumia kiasi cha euro milioni 115 kumrudisha Romelu Lukaku kwenye Ligi Kuu.

Miongoni mwa sajili nyingine zilizotumia fedha nyingi ni pamoja na PSG waliomnunua Achraf Hakimi kwa euro milioni 60, huku Bayern Munich ikitumia euro milioni 42.5 kumsajili Dayot Upamecano.

Makala haya yanaangalia Ligi 10 zilizotumia fedha nyingi zaidi kwenye usajili kwa msimu 2021-22, twende sasa...

### #10. SERIE B (ITALIA) – EURO MIL. 50

Serie B (Ligi Daraja la Pili Italia) ni moja ya ligi iliyotumia fedha nyingi kwa msimu huu wa usajili wa kipindi cha majira ya joto 2021-22.

Kwa ujumla imetumika euro milioni 50, kwa klabu za ligi hiyo ya pili kwa ukubwa nchini Italia.

Parma imetumia kiasi cha karibia euro milioni 30, huku Mfaransa Wylan Cyprien ni moja ya sajili zao kubwa, lakini atatumia msimu huu wa 2021-22 akicheza kwa mkopo kule Nantes.

Hiyo inaonyesha kwamba, Parma, ambayo ilishuka daraja msimu wa 2020-21 kutoka Serie A, inaweza kurudi Ligi Kuu haraka.

### #9. SPL (SAUDI ARABIA) – EURO MIL. 50.2

Ligi Kuu ya Saudi Arabia, (SPL) ni moja ya ligi tajiri katika soka la Asia. Pia, inaweza kuwa ndio ligi yenye ushindani zaidi katika bara hilo.

Klabu za SPL kwa ujumla wake zimetumia kiasi cha euro milioni 50.2 kipindi hiki cha majira ya joto, huku mabingwa wenye rekodi, Al Hilal wakiongoza baada ya kutumia euro milioni 19.8. Mabingwa hao watetezi wametumia euro milioni 18 kumsajili winga Matheus Pereira kutoka West Bromwich Albion, ambaye alishuka daraja la timu yake kutoka kwenye Ligi Kuu England, msimu wa 2020-21.

Usajili mwingine kwenye ligi hiyo ni Igor Coronado kutoka Sharjah FC kwa euro milioni 10.5 na Talisca kutoka Guaz FC kwa euro milioni 8.

### #8. LIGA BWIN (URENO) – EURO MIL. 71.6

Kwa miaka, Ligi ya Kuu ya Ureno imekuwa ikichukuliwa kama mbio za farasi wawili kati ya Porto na Benfica. Na hivyo ndivyo inavyoonekana kwa msimu huu wa 2021-22 kutokana na namna walivyotumia kwenye usajili.

Porto na Benfica, ambao walizimwa na Sporting Lisbon iliyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliopita, wanaonekana kutaka kufufuka. Klabu hizo mbili zimetumia karibia asilimia 60 ya jumla ya kile kilichotumika kwenye usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto kwenye ligi hiyo.

Mshambuliaji mpya wa kati wa Benfica, Roman Yaremchuk ametumia euro milioni 17.5, ambaye ametua hapo akitokea Gent, na amekuwa mmoja wa wachezaji ghali zaidi kutua kwenye Ligi ya Ureno kwa msimu wa 2021-22 hadi sasa.

### #7. JUPILER PRO LEAGUE (UBELGIJI) – EURO MIL. 74.3

Tangu msimu wa 2020-21, mabingwa wa Ubelgiji, Club Brugge wamekuwa moja ya timu zinazotumia fedha nyingi sana kwenye usajili. Hata hivyo, Antwerp wametumia euro milioni 18.8, huku Brugge wakitumia euro milioni 16 kwa msimu wa 2021-22.

Mlinzi wa kati, Stanley Nsoki ametumia euro milioni 6.5, akiwa amesajiliwa na Club Brugge akitokea kwa miamba wa Ligue 1, Nice, na ndio usajili ghali zaidi kwa msimu huu kwenye Ligi Kuu ya Ubelgiji.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ametokea PSG kabla ya kutumia msimu wa 2020-21 akicheza Nice.

### #6. PREMIER LIGA (URUSI) – EURO MIL. 90.6

Zenit St. Petersburg imekuwa iking'ara zaidi kwenye Ligi Kuu ya Urusi baada ya msimu uliopita kutwaa taji la Ligi Kuu kwa mara ya tatu mfululizo.

Kwa kuendeleza umwamba wao, Zenit imefanya usajili wenye thamani ya euro milioni 15.25 kipindi hiki cha majira ya joto, wakimleta kiungo mshambuliaji, Claudinho kutoka Bragantino kwa euro milioni 12.

Kuban Krasnodar imetumia euro milioni 30 kipindi hiki cha majira ya joto, wakimsajili mshambuliaji Jhon Cordoba kwa euro milioni 20 akitokea Hertha Berlin.

### #5. LALIGA (HISPANIA) – EURO MIL. 152.3

Katika hali isiyo ya kawaida klabu kubwa za Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid na Barcelona wametumia jumla ya euro milioni tisa tu kwenye usajili wao hadi sasa. Bingwa mtetezi, Atletico Madrid anaongoza kwa kutumia euro milioni 35.

'Rojiblancos' wametumia kiasi hicho kwa mchezaji mmoja tu ambaye ni mshindi wa Copa America 2021, Rodrigo De Paul. Inaonekana ni timu ambayo itakuwa tena na makali zaidi msimu huu nchini Hispania. Real Madrid ilipata huduma ya mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, David Alaba na Barcelona ikawaleta Memphis Depay, Sergio Aguero na Eric Garcia - wote wakitua hapo kwa uhamisho huru.

Klabu nyingine iliyotumia fedha nyingi kwenye LaLiga msimu huu ni Villarreal (euro Mil 31) na Sevilla (Euro Mil 16.5).

### #4. LIGUE 1 (UFARANSA) – MIL. 301.1

Sio jambo la kushangaza kuona kwamba, miamba wa Ligue 1, PSG ndio waliotumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha kwenye usajili kipindi hiki cha majira ya joto kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa (Euro Mil. 76).

Hata hivyo, wamepata wachezaji wanne bora kabisa duniani kwa uhamisho huru, Lionel Messi, Sergio Ramos, Gianluigi Donnarumma na Georginio Wijnaldum.

Timu nyingine zilizotumia fedha nyingi ni Rennes (Euro Mil. 52.5), Marseille (Euro Mil. 44.7), Monaco (Euro Mil. 34.5n).

### #3. BUNDESLIGA (UJERUMANI) – EURO MIL. 340.3

Bayern Munich ni bingwa mara tisa mfululizo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na wanaonekana wanaweza kulitwaa tena msimu huu.

Wamemsajili Dayot Upamecano (Euro Mil. 42.5) baada ya kuondoka kwa David Alaba kwa uhamisho huru akitua kule Real Madrid.

Klabu tatu, Leipzig (Euro Mil. 91.6), Borussia Dortmund (Euro Mil. 45) na Bayer Leverkusen (Euro Mil. 45.5).

### #2. SERIE A (ITALIA) – EURO MIL. 446.6

Timu za Serie A kwa ujumla wake zimetumia kiasi cha euro milioni 400 kwa kipindi hii cha usajili wa majira ya joto. Lakini cha kushangaza bingwa mtetezi, Inter Milan na Juventus sio miongoni mwa timu zilizotumia kiasi kikubwa cha fedha.

Baada ya kumwachia straika wao, Romelu Lukaku, Inter haijaongeza mshambuliaji, licha ya kufanya usajili wenye thamani ya euro milioni 31.

Timu zilizofanya usajili mkubwa ni AS Roma (Euro Mil. 97.8), AC Milan (Euro Mil. 58.1) na Atalanta (Euro Mil. 47).

Straika wa Chelsea, Tammy Abraham ametua Roma kwa euro milioni 40 na ndio umekuwa usajili ghali kwenye Serie A msimu huu.

### #1. PREMIER LEAGUE (ENGLAND) – EURO BILIONI 1.02

Katika sajili nne kubwa kati ya tano kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto, tatu za juu zimefanywa na klabu za Ligi Kuu ya England. Jack Grealish (Euro Mil. 117.5), Romelu Lukaku (Euro Mil. 115) na Jadon Sancho (Euro Mil. 85).

Klabu za Manchester City, Chelsea na Manchester United ndizo zilizotumia kiasi kikubwa zaidi cha fedha.

Kwa ujumla Manchester City (Euro Mil. 127.5), Manchester United (Euro Mil 125 - Dau hilo kabla ya usajili wa Cristiano Ronaldo), Chelsea (Euro Mil. 115) na Aston Villa (Euro Mil. 105.6).

Timu kama Arsenal, Leicester City nazo hazijasita kutumia kiasi kikubwa cha fedha.

## Nukuu

"Cristiano ameitumikia Juventus kwa kipindi cha miaka mitatu, amefunga mabao, kitu ambacho ni kizuri sana, ni mchezaji wa kipekee, lakini hatuwezi kufikiria kuhusu Ronaldo kuanzia sasa na kuendelea. Nina kikosi kizuri, lazima tutambue kuwa hatuwezi kutawala kila mechi," **Kocha Mkuu wa Juventus, Massimiliano Allegri, baada ya juzi kuangukia pua ya bao 1-0 dhidi ya Empoli katika Uwanja wa Turin.**



"Sidhani kama klabu hii katika historia yake imewahi kukumbana na jambo hili. Tunatakiwa kukabiliana na changamoto. Ligi na msimamo huwa hauamuliwi Agosti. Kitu kibaya unachoweza kufanya ni kurusha taulo. Hatuwezi kufanya hivyo," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta ambaye juzi timu yake ilichapwa mabao 5-0 na Man City.**



"Ni habari kubwa kwa kila mtu kusikia kwamba Kane anabaki, tutafanya vizuri na tutafanya naye kazi leo tukiwa na uhakika wa uwapo wake kesho, hilo limeisha," **Kocha Mkuu wa Tottenham, Nuno Espirito Santo.**



# NANI YUPO WAPI, USAJILI LIGI KUU BARA UKIFUNGWA KESHO



NDEMLA

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imebaki siku moja tu kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa msimu huu wa 2021/22, kumekuwa na harakati kubwa za klabu za Ligi Kuu kuchukua wachezaji huku na huko kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano hayo.

Zipo zinazosajili kwa ajili ya Ligi Kuu, Kombe la FA na mashindano mengine ya ndani. Lakini kuna timu kama Simba, Yanga, Azam FC na Biashara zenyewe zimeenda mbali zaidi kwani zinasajili pia kwa ajili ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Hivi sasa tunashuhudia wachezaji wa klabu hii wakitua klabu nyingine. Huyu anatoka huku kwenda kule. Yule anatoka kule kwenda huku, ili mradi mwenye kisu kikali ndiye anayekula nyama.

Kesho saa 5:59, Shirikisho la Soka nchini (TFF), litafunga dirisha la usajili. Kwenye makala haya tutawaangaza wachezaji ambao mpaka sasa wamesajiliwa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu na kuthibitisha usajili huo. Tutaowaangalia hapa ni wachezaji wa Kitanzania tu ambao wametoka klabu moja kwenda nyingine.

**#1. HAMISI NDEMLA - MTIBWA SUGAR**

Baada ya kukaa kwa miaka mingi, hatimaye kiungo huyu mwenye mashuti makali, ameondoka klabu ya Simba na kwenda kujiunga na Mtibwa Sugar.

Ndemla, ambaye anacheza kiungo mshambuliaji na wakati mwingine kiungo mkabaji, amepelekwa kwa mkopo na klabu yake ya Simba na sasa kwa mara ya kwanza ataonekana akiwa amevaa jezi tofauti na klabu ambayo aliichezea tangu akiwa kikosi cha pili mwaka 2012 hadi alipopandishwa kikosi cha wakubwa 2013.

**#2. DICKSON AMBUNDO - YANGA**

Ni kiungo mshambuliaji ambaye msimu huu ataonekana akiwa amevaa jezi ya njano na kijani. Ambundo ambaye alitamba msimu uliopita akiwa na klabu ya Dodoma Jiji, alivutia makocha mbalimbali wa Ligi Kuu, akiwamo Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes ambaye alimsifia hadharani. Inawezekana ikawa ndiyo sababu ya Yanga kumuwahi.

**#3. ABDULSWAMAD KASSIM - SIMBA**

Anacheza kama kiungo mkabaji. Wakati mwingine pia anacheza kama kiungo mshambuliaji, amesajiliwa na Simba msimu huu akitokea Kagera Sugar. Ni mchezaji ambaye anaichezea timu ya Zanzibar Heroes, na ndiye anaonekana kwenda kuziba nafasi ya Ndemla kwenye kikosi cha Simba na kuleta changamoto kwa wengine.

**#4. JUMA MAHADHI - GEITA GOLD**

Amejiunga na Geita Gold baada ya kumaliza mkataba wake wa mkopo kwenye klabu ya Ihefu akitokea Yanga.

Mahadhi ambaye alisajiliwa na Yanga kutoka Coastal Union, alionekana zaidi kwenye chumba cha daktari badala ya uwanjani. Alipopona akapelekwa Ihefu kwa mkopo, mkataba wake na Yanga umemalizika na sasa ni mchezaji halali wa Geita Gold.

**#5. JIMMYSON MWANUKE - SIMBA**

Kijana kutoka Gwambina, amejiunga na klabu ya Simba. Mwanuke mwenye miaka 18, anamudu nafasi ya kiungo mshambuliaji na wakati mwingine hucheza kama winga. Ni mchezaji mwenye uwezo wa kuuchezea mpira na mashuti makali.

**#6. YUSUPH ATHUMANI - YANGA**

Kiungo mshambuliaji, ambaye ana uwezo wa kucheza kama kiungo mkabaji. Yanga imemsajili mchezaji huyo kutoka Biashara United na ni mmoja wa wachezaji wanaotarajia kufanya makubwa kwenye kikosi hicho.

**#7. IBRAHIM AME - MTIBWA SUGAR**

Beki huyu wa kati amekwenda klabu ya Mtibwa kwa mkopo akitokea Simba. Ame ambaye alisajiliwa na Simba msimu uliopita kutoka Coastal Union, hakupata nafasi kubwa ya kucheza msimu uliopita. Kwa usajili wa msimu huu, ikaonekana aondoke akapate nafasi ya kucheza.

**#8. ISRAEL MWENDA - SIMBA**

Ametoka kwenye klabu ya KMC na sasa amejiunga na Simba. Anaonekana kwenda kumpa changamoto Shomari Kapombe ambaye pamoja na kuwa ana kiwango kizuri, lakini ni mchezaji mwenye majeraha ya mara kwa mara, kiasi kwamba anapoanguka chini na kuumia, mioyo ya mashabiki wa Simba inakuwa juu.

**#9. DAVID KAMETA - BIASHARA UNITED**

Hakumpa changamoto yoyote Kapombe upande wa beki wa kulia. Pamoja na kwamba kiwango chake ni kizuri, lakini mashabiki wengi wa Simba waliona kama anacheza kitoto zaidi. Ujio wa Mwenda umeifanya klabu ya Simba kumpeleka Biashara United kwa mkopo.

**#10. MESHACK ABRAHAM -KAGERA SUGAR**

Ni straika aliyetikisa msimu uliopita akiwa kwenye klabu ya Gwambina. Alimaliza akiwa na mabao tisa, awali ilionekana kama angetua kwenye klabu kubwa zaidi, lakini haikuwa hivyo na Kagera Sugar imeweka mzigo mkubwa na kupata saini yake.

**#11. BENEDICT HAULE - PRISONS**

Kama unamkumbuka kipa huyu, msimu uliopita aliidakia Azam FC. Msimu ujao atasimama kwenye milingoti mitatu ya kikosi cha Prisons. Anakwenda kuchukua nafasi ya Jeremiah Kisubi ambaye mpaka wakati huu haijajulikana amesajili timu gani.

**#12. KELVIN NAFTARI - GEITA GOLD**

Mashabiki wengi wanamfahamu kuwa ni kiungo mkabaji mtundu na mkorofi akiwa uwanjani. Wengi walizoea kumwona akiwa na JKT Tanzania, tangu wakati huo ikiitwa JKT Ruvu. Kwa mara ya kwanza msimu ujao ataonekana akivaa jezi za Geita Gold.


**#13. EMMANUEL MARTIN - DODOMA JIJI.**

Anakumbukwa sana kuwa alikuwa straika wa Yanga kwa misimu kadhaa nyuma. Msimu uliopita alichezea Ruvu Shooting na kufunga bao timu yake ya zamani ya Yanga. Na amekuwa akifanya hivyo mara kwa mara kuifunga Yanga kila timu anayohamia. Amejiunga na Dodoma Jiji.

**WENGINE**

Wengine ni Hassan Kibailo aliyetua Mtibwa Sugar akitokea Coastal Union, Mohamed Yusuph (Dodoma Jiji) kutoka Polisi Tanzania, Benedict Tinoco (Geita Gold) akitoka kuitumikia Kagera Sugra, Gerald Mgeveke-(Dodoma Jiji) akitokea Mwadui FC, Yusuph Abeid (Kagera Sugar) kutoka Namungo FC, Hassan Nassor (Dodoma Jiji) akitoka Polisi Tanzania na Amos Kadikilo (Geita Gold) kutoka Gwambina FC.

**JE, WAJUA?**



KWA mara ya kwanza katika historia ya Arsenal kwenye Ligi Kuu England imepoteza mechi tatu mfululizo bila ya kufunga hata bao moja. Lakini kadi nyekundu alioonyeshwa Granit Xhaka wakati wakifungwa mabao 5-0 na City juzi, ni ya 10 kwa wachezaji wa klabu hiyo tangu kocha Mikel Arteta aanze kuinoa Desemba 2019.





## Askofu aipa neno serikali kuhusu chanjo ya corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU Katibu Mkuu wa Kanisa la PHAMT, Askofu Julias Bundala, ameishauri serikali kuendelea na msimamo wake wa utoaji chanjo ya UVIKO-19 kuwa ni hiari na siyo lazima.

Bundala aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Askofu huyo alisema kuwa ni vizuri serikali kusimamia pale ilipotoa maamuzi yake ya kuwataka watu kushiriki kwa hiari kwa kila mtu anayetaka kuchanja au kutochanjwa ili kuwapa uhuru.

"Mtu kama hajachanjwa au hataki kuchanjwa asishtumiwe, kwa sababu ana uhuru wa maamuzi yake na ukizingatia tayari serikali imeshasema kuchanjwa ni hiari," alisema.

Aidha, aliwaomba wataalamu wa afya kwa kushirikiana na viongozi wa dini, kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania dhidi ya ugonjwa huo wa corona.

Alisema kuna kila sababu kwa wataalamu wa afya pamoja na viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu kwa jamii kwa ajili ya kuwaweka katika tahadhari ya jinsi ya kujilinda na corona.

Askofu huyo aliomba Watanzania kuendelea kumtegemea Mungu kwenye kuliondoa janga hilo.

Alisema kuwa katika kipindi cha uwapo wa ugonjwa huo, Watanzania wanatakiwa kushirikiana kwenye maombi ili Mungu awanusuru na ugonjwa huo.

# Serikali yahamasisha matumizi ya tiba asili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imewahamasisha wananchi umuhimu wa matumizi ya tiba asili katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo UVIKO-19.

Uhamasishaji huo ulifanyika jana kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Aya Mwafrika ambayo kilele chake ni Agosti 31.

Akizungumza katika utoaji elimu ya matumizi ya tiba hiyo, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Tiba Mbadala, Dk. Vumilia Liggie, alisema kuwa, wataalamu wa tiba hiyo wametembelea hospitali na vituo vya afya ili kuzungumza na wagonjwa na kuwapa elimu kuhusu umuhimu wa tiba asili katika mapambano dhidi ya magonjwa mbalimbali nchini.

"Kwa siku ya leo tumetembelea vituo vya afya vitatu, tumetembelea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma General kama kituo cha kwanza, ambapo tumeenda sehemu ya wagonjwa wa nje wa hospitali ambapo tumeweza kuzungumza na wagonjwa na kuwapa elimu kuhusu tiba asili," alisema.

Alibainisha Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Namba 23 ya Mwaka 2002 iliyopitishwa na Bunge.

"Baraza hili ndio linasajili dawa, waganga wa tiba asili, na kuwajua wako wapi na wanafanya nini, na kuhakikisha dawa hizo ni salama kwa matumizi ya binadamu na linashirikiana na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, maabara ya TMDA, maabara ya taasisi ya dawa asili pamoja na Maabara ya Shirika la viwango Tanzania," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Shirika la Dawa Asilia na Ulinzi wa Mazingira, Boniventura Mwalongo, alieleza zaidi ya asilimia 93 ya dawa zinaagizwa kutoka nje ya nchi, hivyo Serikali imelenga kuboresha tafiti za ndani, kuongeza uzalishaji wa ndani ili kutoa fursa za ajira, hususan kwa vijana, hivyo kupitia kuikuza tiba asili nchini yote yanawezekana.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Waganga wa Tiba Asili, Dk. Elizabeth Lema, alisema maadhimisho hayo yanatoa fursa kwa waganga wa tiba asili na tiba mbadala kuonyesha bidhaa zao mbalimbali ambazo tayari zimesajiliwa kupitia baraza na kuthibitishwa kuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Alitoa rai kwa wananchi kuhudhuria maonyesho hayo yatayofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (kulia), akishauriana jambo na Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma , Prof. David Mwamfupe (kushoto) pamoja na Mkuu wa Wilaya, Jabir Shekimweri (katikati), walipokutana mwisho wa wiki jijini humo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Mashimba aagiza matumizi mfumo ukaguzi wa mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameagiza mfumo wa ukaguzi wa mifugo na mazao yake kutumika kwa ufanisi huku akiwaonya wakaguzi kutogeuka kuwa Jeshi la Polisi.

Ndaki alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokuwa akizindua mfumo huo unaolenga kuongeza tija na kuinua pato la taifa kupitia sekta ya mifugo.

Alisema mfumo huo ni rahisi na ushirikishwaji hivyo ni vyema wakaguzi kutogeuka kuwa Jeshi la Polisi na kuwasumbua wadau wa sekta ya mifugo.

Aliwataka wakaguzi kutumia mfumo wa ukaguzi wa mifugo na mazao yake kuhakikisha sheria, kanuni, taratibu za kusimamia na udhibiti wa ubora, usalama na viwango stahiki vinasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo.

"Utaratibu huu ni wa ushirikishwaji, sasa tunapokuwa huko kufanya ukaguzi kuhusiana na ubora na viwango tusijigeuze sisi kuwa polisi. Kwa nchi yetu mfumo huu ni rahisi na ambao umelenga kuzipatia taarifa wizara, taasisi na wadau wengine kuhusiana na ukaguzi, ubora na usalama wa mifugo pamoja na mazao yake," alisema.

Alisema umuhimu wa mfumo huo ni kuhakikisha utekelezaji wa wajibu wa kulinda afya za walaji, mifugo na mazao yake kwa kusimamia sheria, kanuni na taratibu jambo ambalo litasaidia wafugaji kuzalisha mifugo kwa tija kwa kutumia pembejeo na huduma zilizosajiliwa na kutambuliwa kisheria.

Alitoa wito kwa wataalamu wa Wizara, Mamlaka za Serikali za mitaa, taasisi na wadau waliopo kwenye vyama vya tasnia kuhakikisha wakaguzi, wazalishaji, watoa huduma kwenye mifugo wanazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo ili kuhakikisha mlaji wa mifugo na mazao yake anaendelea kunufaika kiafya na kimaslahi kupitia maziwa, nyama na mayai na bidhaa nyingine.

Waziri Ndaki aliwaomba wafugaji wote nchini kujenga utamaduni wa kutumia pembejeo na malighafi zenye ubora, usalama, viwango stahiki kutoka kwenye vyanzo vilivyosajiliwa kwenye uzalishaji wa mifugo.

"Hatua hii muhimu itasaidia upatikanaji wa bidhaa bora zinazozalishwa, kuchakatwa na kukaguliwa na wataalamu wa mifugo hapa nchini," alisema.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Miugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Amosy Zephania, alisema wizara imeanzisha na kuboresha mfumo wa ukaguzi wa mifugo na mazao yake ambao umejikita kwenye tasnia za kuku, maziwa, nyama, mayai, ngozi, malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo.

Alibainisha kuwa mfumo huo umeanishwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia mradi wa maboresho ya ufugaji kibiashara (L-MIRA) ambao umewezesha kufanyika mapitio ya sheria tatu za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama ya mwaka 2010, Magonjwa ya Wanyama ya mwaka 2003 na Sheria ya Veterinari ya mwaka 2003 na kanuni 12.

Zephania alisema mfumo huo umelenga kuongeza ari na hamasa ya uwekezaji kwenye sekta ya mifugo kwa kutatua kero za ubora, usalama na viwango stahiki kwenye mifugo, mazao ya mifugo na pembejeo za mifugo.





# Kalemani aagiza vijiji visivyo na umeme viunganishwe

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amezindua mradi wa usambazaji wa umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu mzunguko wa pili huku akiagiza vijiji na vitongoji vyote vya Mkoa wa Mbeya ambavyo havikuunganishiwa huduma hiyo awamu zilizopita viunganishwe.

Alizindua mradi huo juzi katika Kijiji cha Kagwina, Kata ya Lufingo, wilayani Rungwe na kusema serikali imetenga Sh. bilioni 40.8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo katika Mkoa wa Mbeya.

Alisema vijiji ambavyo umeme ulishafika kupitia awamu zilizopita za REA, lakini baadhi ya nyumba zilirukwa upo mradi mwingine ambao unaendelea wa kujaziliza nishati hiyo ili kila nyumba ipate umeme.

Aliagiza kwa mujibu wa mkataba wa mradi huo, vijiji vyote vinatakiwa viwe vimewashiwa umeme kufikia mwezi Desemba mwaka 2022 huku akiagiza viongozi wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), kwa kushirikiana na REA wahakikishe wanawasimamia makandarasi.

Dk. Kalemani aliwataka makandarasi wafanye kazi usiku na mchana kwenye vijiji ili wakamilishe shughuli hizo mapema huku akiwataka kuanza na Kata ya Lufingo alipozindulia mradi huo wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili.

"Nataka muanzie kwenye kijiji hiki cha Kagwina na natoa siku 15 kuanzia leo umeme uwake kwenye kijiji hiki, naweza nikaja mimi mwenyewe ama nitatuma mtu, lakini nataka umeme uwake hapa haraka sana, nimeambiwa kuwa kutoka ofisi za TANESCO mpaka hapa ni kilomita 10 sasa fungueni ofisi ndogo hapa wananchi walipie," alisema Dk. Kalemani.

Alisema gharama za wananchi kuunganishiwa umeme kwenye nyumba zao ni Sh. 27,000 na hawatakiwi kulipia nguzo na kuwataka watumishi wa REA na TANESCO kuepuka mtego wa kuanza kuwatoza wananchi gharama za ziada kwa kuwa watashughulikiwa.

Vilevile, aliwataka mameneja wa TANESCO wa mikoa na wilaya kushughulikia matatizo ya umeme kukatika katika ili kuondoa malalamiko miongoni mwa wananchi na kuruhusu shughuli za uzalishaji kuendelea.

Pia alitoa miezi miwili kwa TANESCO na REA kuunganisha umeme kwenye vijiji 25 vya Wilaya ya Rungwe ambavyo vilirukwa kwenye awamu ya pili ya REA.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Nkondo Bendera, alisema katika wilaya hiyo vipo vijiji 34 ambavyo havikuunganishwa umeme kwenye awamu zilizopita na kwamba kwenye awamu inayoendelea sasa ni kijiji kimoja pekee ndicho hakikuingizwa.

Alisema serikali ya wilaya hiyo itahakikisha inashirikiana na TANESCO na REA kuwasimamia makandarasi wanaofanya kazi kwenye vijiji ili kuhakikisha umeme unavifikia vijiji vyote ambavyo vipo kwenye mradi huo.

Alisema mpaka sasa kwa upande wa Halmashauri ya Busokelo ni kijiji kimoja pekee kisichokuwa na umeme na kwa upande wa Busokelo ni vijiji 33 na.

"Kwa takwimu hizo ni kwamba kwa Busokelo tumefikia zaidi ya asilimia 90 lakini huku Rungwe tupo asilimia 75 na naamini kwa awamu hii tutafikia asilimia 100," alisema Bendera.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ismail Mlawa, ambaye alimwakilisha Mkuu wa wilaya hiyo, alisema nishati hiyo ya umeme ni muhimu kwenye shughuli za wananchi.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akiwakabidhi kifaa cha umeme tayari (UMETA) baadhi ya wazee wa Kitongoji cha Kipapa kilichoko Kata ya Lufilyo, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme kwenye vijiji unaotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TSF, TANAPA watakiwa kushirikiana kuepusha uharibifu wa mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATENDAJI wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) na wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), wametakiwa kushirikiana kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye maeneo wanayosimamia ili hatua za kuyanusuru maeneo hayo zichukuliwe.

Aidha, watendaji wa taasisi hizo wametakiwa kuwasilisha serikalini mapendekezo ya namna bora ya kudhibiti tatizo hilo la uharibifu wa mazingira ili utatuzi wa matatizo hayo kwenye maeneo ya hifadhi utakaochukuliwa uwe ni suluhu ya kudumu.

Agizo hilo lilitolewa na wakuu wa wilaya za Mbeya na Songwe wakati wa kikao cha pamoja na maofisa wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, pamoja na maofisa misitu wa halmashauri kilichokuwa na lengo la kujadili hali ya uharibifu wa mazingira kwenye misitu inayosimamiwa na wakala huo.

Vilevile, kikao hicho kililenga kujadili namna bora ya uvunaji wa misitu pamoja na biashara ya mazao ya misitu ili ifanyike kwa tija bila kuharibu mazingira na kusababisha migogoro isiyokuwa na tija baina ya TFS na wananchi wanaozunguka misitu ya hifadhi.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon alisema kumekuwa na shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya misitu ambazo zinasababisha uharibifu mkubwa wa misitu hiyo pamoja na rasilimali zingine.

Alisema kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakiingiza makundi makubwa kwenye mitistu ya hifadhi, kuchimba madini kwenye misitu hiyo pamoja na kuanzisha mashamba makubwa kwenye maeneo ya hifadhi shughuli ambazo alisema ni hatari kwa ustawi wa misitu hiyo.

"Ni vyema kabla hatujaanza kutafuta njia za kutatua matatizo haya, ifanyike kwanza tathmini ya makusudi kwenye misitu hiyo ili tunapotafuta njia ya kunusuru misitu yetu tuwe na uhakika wa kile tunachokifanya," alisema Mayeka. Naye Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Cosmas Nshenye, alisema baada ya tathmini hiyo kufanyika waangalie uwezekano wa kuimarisha ulinzi kwa kutumia vikundi vya jeshi la akiba kulinda misitu hiyo.

Alisema wapo vijana wengi ambao wana mafunzo ya mgambo, lakini hawana shughuli za kufanya na kutaka waunde vikundi ambavyo vitawezeshwa kuanzisha shughuli za kiuchumi ili vilinde misitu hiyo dhidi ya waharibifu.

"Tunaweza tukaviwezesha kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki ama ufugaji wa samaki, hii itasaidia vijana hao kujiingizia kipato na wakati huo wakilinda misitu isivamiwe na wahalifu, wilaya zetu zina misitu mingi na muhimu sana, lakini tusipoilinda itakwisha," alisema Nshenye.

Kwa upande wake Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alisema waliamua kufanya kikao hicho ili wawe na kauli ya pamoja kwenye utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na kuepusha migongano.

# TARI yabaini tatizo tindikali kwenye udongo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), umebaini kuwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za juu Kusini inakabiliwa na tatizo la tindikali kwenye udongo hali inayoathiri uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na mtaalamu wa utafiti wa udongo kutoka TARI, kituo cha Uyole jijini hapa, Fredrick Mlowe, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi sahihi ya ardhi kuelekea msimu mpya wa kilimo.

Alisema kwenye utafiti walioufanya walibaini kuwa mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inakabiliwa na tatizo hilo hali inayosababisha wakulima wengi kuzalisha mazao yasiyoendana na ukubwa wa mashamba.

Aliwataka wakulima kupima afya ya udongo kabla ya kuanza kuzalisha zao lolote na huduma hiyo inapatikana kwenye maabara ya kituo hicho na uwapo wa tindikali nyingi kwenye udongo hauruhusu mazao kustawi.

"Uwapo wa tindikali katika udongo nyingi kwenye udongo husababisha wakulima kupata hasara ya mazao kukauka au mavuno duni hivyo tumeamua kutoa elimu kwa wakulima namna ya kukabiliana na hali hiyo na njia ya kuikabili hali hiyo ni kutumia chokaa," alisema Mlowe.

Aliongeza kuwa mimea mingi haistahimili kukua kwenye udongo wa tindikali isipokuwa zao la chai pekee na kwamba wanaendelea kuwaelimisha wakulima kupima udongo kupitia maabara zilizopo.

Mkurugenzi wa Kilimo kutoka Shirika la Kilimo Afrika (The Nature Conservancy), Felix Kamau, alisema wakulima wadogo nchini huwa wanakata tamaa wanapopata mavuno hafifu wakiamini kuwa hali hiyo inasababishwa na kutotumia mbolea ya kutosha jambo ambalo alidai sio kweli.

Aliwataka wakulima kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo kabla ya kuzalisha zao lolote na kwamba wanapobaini kuwa mazao yao hayakui ni vyema wakawasiliana na wataalamu ili washauriwe cha kufanya.

Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliwataka wakulima wa kanda hiyo kutumia kituo hicho kupata mbinu za kilimo bora ili waongeze tija kwenye uzalishaji.

# Wadau wajadili athari mabadiliko tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, amesema mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakiathiri dhana nzima ya mipango miji na vijiji.

Amesema hali hiyo imekuwa chanzo cha majanga mbalimbali ambayo yamekuwa yakijitokeza duniani kote.

Aliyasema wakati wa ufunguzi wa kongamano la kujenga uhimili wa mabadiliko ya tabianchi ambalo lilijumuisha wadau kutoka sekta mbalimbali ambao ni walengwa wa kukabiliana na maafa lililotayarishwa na Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania Kanda ya Zanzibar.

Alisema lengo la kikao hicho ni majadiliano kwa wadau husika wenye kusimamia mradi wa uhimili katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi ili kuleta mafanikio kwa wananchi wa Zanzibar.

Alizitaka taasisi zinazosimamia mradi huo kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuona mafanikio yanawanufaisha wananchi wa Zanzibar kwa msingi wa kuepukana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi huyo alilishukuru Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kuunga mkono mradi huo, ambao umeonyesha utakuwa na matokeo mazuri nchini.

Mada tatu ziliwasilishwa na kujadiliwa katika kongamano hilo ikiwamo masuala ya hali ya hewa katika kamisheni ya kukabiliana na maafa, mikakati ya pamoja juu ya utoaji wa tahadhari za mapema za maafa pamoja na masuala ya mazingira na hali ya hewa.

# Daktari afunguka tatizo la kukojoa kitandani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI wa magonjwa ya akili katika Hospitali ya Kidongo Chengundu Zanzibar, Khadija Abdulrahman omar, amewataka watu wenye tatizo la kukojoa kitandani kutoona aibu kwenda hospitalini hapo kufuata matibabu kwa sababu huo ni ugonjwa.

Akizungumza na Nipashe jijini Zanzibar, alisema tatizo hilo ni maradhi kama yalivyo maradhi mengine, hivyo ni vyema kufuata tiba haraka.

Alisema mtu aliyefikia umri wa miaka sita na kuendelea ambaye anakojoa kitandani ana tatizo la kiafya na anahitaji kupata tiba haraka.

Alisema tatizo hilo lipo, lakini watu wengi wanaona aibu kufuata huduma za matibabu hospitalini kutokana na kunyanyapaliwa katika familia zao.

"Wapo ambao wanakumbana na kipigo kutoka kwa familia zao na wengine hata kutoka kwa waume zao kutokana na kukojoa kitandani...ufahamu kuwa kikojozi anahitaji tiba kama mgonjwa wa maradhi mengi," alisema.

Alisema hospitalini hapo wanapokea wagonjwa 50 kwa mwezi ambao ni wa rika tofauti ambao wengi wao waliovuka miaka 14 na kuendelea na baadhi ya wenye tatizo hilo huwa wanaathirika kisaikolojia, kutokana na unyanyapaa na wengine huacha hata shule kutokana na kuwa na tatizo hilo.

Dk. Khadija alieleza kukojoa kitandani kunachangiwa na sababu mbalimbali ikiwamo magonjwa ya kisukari, kifafa, maradhi ya akili na wengine huwa ni urithi.

Aidha, alisema baadhi ya wagonjwa wa akili chanzo chao hutokana na kukojoa kitandani na hatimaye hupata msongo wa mawazo kutokana na kunyanyapaliwa na wengine hukutana na vipigo katika familia zao.

Daktari huyo aliwashauri wenye tatizo hilo kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu wa afya ikiwamo kutopendelea kula chakula nyakati za usiku na kuweka alam katika simu zao nyakati za usiku ili kupata muda wa kwenda chooni kwa sababu ugonjwa huo unatibika.

Alisema utamaduni wa uvalishwaji wa pampasi kwa watoto kunachangia kuongezeka kwa idadi ya vikojozi, kwa sababu katika ukuaji wa mtoto kiakili anatakiwa kwenda chooni mwenyewe umri kuanzia miaka miwili.

Alisema mtoto kuanzia miaka miwili anatakiwa kupewa elimu ya huduma ya choo, lakini kutokana na uvivu wa wazee na walezi mtoto wa miaka minne bado anavalishwa pampasi.

Alisema vikojozi wanaofuata huduma za afya hospitalini hapo hupatiwa tiba na wengi wao hupona kabisa.



Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud, akizungumza na wafuasi wa Chama cha ACT-Wazalendo alipotembelea Kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tamasha lachochea watu kupata chanjo corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI mbalimbali wametumia fursa ya kupata chanjo ya corona katika tamasha la Kizimkazi ambalo lilifungwa jana na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi waliofika katika tamasha hilo na kupata chanjo ya corona walisema kuwa siku mbili zilizotengwa kwa ajili ya chanjo ya corona katika tamasha hilo ni chache kwa sababu baadhi yao hawakuwa na taarifa ya utoaji wa chanjo hiyo.

Sinajambo Mkonde Makame, mmoja wa wananchi waliochanja katika tamasha hilo, alisema ameshawishika baada ya kuona watu wengi wamejitokeza kuchanja, hivyo akamua na yeye kuitumia fursa hiyo.

Sinajambo ambaye ni mjasiriamali, alisema mwanzoni alikuwa na hofu kuhusu chanjo ya corona kutokana na kasumba mbalimbali zinazotolewa na baadhi ya watu kuhusu chanjo ya corona.

"Natoka nyumbani sikuwa na nia kabisa ya kuchanja chanjo ya corona, lakini baada ya kufika hapa nimeshawishika na tayari nimeshachanja, hivyo nawaomba wananchi wenzangu kwenda kuchanja ili kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema Sinajambo.

Alisema kwa kuwa tamasha la Kizimkazi limeshafungwa kwa mwaka huu, ni vyema wananchi kuifuata chanjo ya corona katika vituo vya afya vilivyotangazwa na serikali ikiwamo Hospitali ya Makunduchi kwa Wilaya ya Kusini Unguja.

Naye Husein Haroub, alisema amefurahia kupata chanjo ya corona ambayo alikuwa ana mpango wa kwenda kuchanja Dar es Salaam, kwa sababu Zanzibar haina chanjo ya corona aina ya Jonson ambayo alikuwa anaihitaji.

"Nimefurahi sana leo hii kuja hapa Kizimkazi katika tamasha na kukuta chanjo inayotolewa ni ya Jonson, maana ingenibidi nigharamike Sh. 50,000 kwa ajili ya nauli ya boti kwenda Dar es Salaam kupata chanjo, lakini leo hii nimeshachanja hapa Kizimkazi bila ya gharama yoyote," alisema.

Aliwataka vijana wezake kutodharau chanjo badala yake kwenda kuchanja ili kujikinga na ugonjwa huo kwa kuwa serikali imeshatangaza kuwa idadi ya wagonjwa wa corona ni wengi katika Hospitali ya Mnazimmoja.

Waziri wa Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, aliwapongeza wananchi waliojitokeza kuchanja katika tamasha la Kizimkazi ambapo siku mbili zilitengwa kwa ajili ya chanjo ya corona.

Alisema kwa wale ambao bado hawajachanja chanjo ya corona serikali ya Zanzibar imetayarisha vituo maalum kwa ajili ya kutoa chanjo hiyo kwa Unguja na Pemba, na kwamba kila mwananchi anayo haki ya kuchanja ambapo vituo hivyo vitaanza kutoa chanjo leo.

Alivitaja vituo hivyo kwa kisiwa cha Pemba ni Wete, Micheweni, Mkoani na Chakechake wakati kwa upande wa Unguja ni Rahaleo, Tunguu, Mahonda, Mpendae, Magirisi, Kivunge, Makunduchi na Hospitali Kuu ya Mnazimmoja.

"Chanjo ni moja katika nyenzo muhimu itakayoweza kupunguza ugonjwa huu nchini tutumie fursa hii ambayo haina malipo twende katika vituo ili tuweze kujikinga na corona," alisisitiza.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Afya aliyoitoa juzi, watu 40 wameshafariki dunia kutokana na corona na 36 wamelazwa katika Hospitali ya Mnazimmoja wanaugua corona ambao wanahitaji oksijeni kwa ajili ya kupumua.

# Ufadhili wa TMEA wanufaisha mamia wanawake kibiashara

**Na Pascal Mayalla**

ZAIDI ya wanawake 200 kutoka katika Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania(TWCC), wamejengewa uwezo wa kuzalisha bidhaa bora kwa ufadhili wa Taasisi ya TradeMark East Afrika(TMEA).

Pia wapatiwa uwezo wa namna ya kufanya biashara zao kwa kufuata sheria na taratibu za biashara ikiwamo kupata nembo zenye ubora wa Mamlaka ya Udhibiti Viwango (TBS) pamoja na barcode na kufanikiwa kushiriki katika maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam na kutangaza biashara zao.

Mkurugenzi Mkazi wa TMEA, Tawi la Tanzania, Monica Hangi, alisema hayo katika mkutano wa kutathmini ushiriki wa TWCC kwenye maonyesho hayo ya Sabasaba mwaka huu.

Hangi, aliipongeza TWCC kwa kazi kubwa waliyoifanya katika maonyesho hayo ikiwamo kufanikisha kukutanisha idadi kubwa ya wafanyabiashara hao wanawake katika maonyesho hayo mwaka huu.

"Ninawapongeza sana TWCC kwa kazi kubwa wanayofanya, kuona wanawake kutoka maeneo mbalimbali wameboresha bidhaa zao kwa vifungashio, packaging na branding, wengi wao sasa wana nembo ya TBS na barcode, sasa wanaweza kuuza bidhaa zao nje ya nchi na wana masoko ya uhakika," alisema Hangi.

"Lengo la TMEA kufadhili wafanyabiashara wanawake, linaanza kutimia, kwa kusupport na kuwasaidia wanawake wa Tanzania kufanya biashara mpaka nje na kupata masoko ya kudumu."

Kwa upande wao, Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Silla, alisema TMEA wametoa msaada mkubwa kwa wanawake hao kufanikisha malengo yao ya kibiashara.

"Jukumu letu lilibaki ni kuhakikisha tuwafikie wanawake wote katika ngazi zote ili kuwawezesha kurasimisha biashara zao, na tunaamini kwa kufanya hivyo tunachangia uchumi wa nchi yetu, lakini pia uchumi wa familia zao kama Rais wetu Samia Suluhu Hassan anavyosisitiza kila mara," alisema Silla.

Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, aliishukuru alisema tayari wamefanikiwa idadi kubwa ya wanawake tangu wameanza kufanya kazi na TMEA.

"Na tuna mradi ambao tumeuanza ambao tunategemea kufikia wanawake elfu 10 kuwasaidia kupata taarifa za kibiashara, kuwajengea uwezo wa biashara zao kukidhi vigezo na viwango vya kuziuza katika masoko ya kimataifa," alisema Mwajuma.

"Pia TMEA wanatutengenezea mfumo kuuza kwa mtandao, kwa hiyo kutokana na janga la corona, wafanyabiashara wanawake wataendelea kuuza bidhaa zao kupitia mitandao kwasababu tayari TradeMark wamefadhili mfumo mpya wa kuuza bidhaa za Tanzania kupitia mtandao."

Kwenye maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam mwaka huu, TWCC ni miongoni mwa mabanda yaliyofanikiwa kutwaa tuzo za mabanda bora.



Mjasiriamali wa TWCC, Rehema Patrick wa Eden Products kutoka Morogoro, akionyesha bidhaa zake kwa Mkurugenzi Mkazi wa Trade Mark East Africa Tawi la Tanzania, Monica Hangi (kulia), wakati wa onyesho maalum la bidhaa za wajasiriamali wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara wa Tanzania, TWCC, kutathmini ushiriki wa TWCC kwenye Maonyesho ya 45 ya Sabasaba juzi, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Atangaza neema umeme shule za msingi/sekondari

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

MKURUGENZI wa kampuni ya kuzalisha na kutibu nguzo za umeme (QWIHAYA), Leonard Mahenda, ametangaza neema kwa shule za msingi na sekondari za wilaya ya Njombe na Ludewa, mkoani Njombe kwa kulipia huduma ya kuunganishiwa umeme wa REA.

Mahenda alitoa ahadi hiyo mbele ya Waziri wa Nishati, Medard Kalemani, wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kuzalisha na kutibu nguzo kilichopo Kata ya Mtwango, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, jana.

Alisema amekuwa akiunga mkono serikali katika kutatua changamoto mbalimbali ikiwamo ya nishati ya umeme wa uhakika.

"Waziri nikuahidi kwamba nitalipia umeme kwa shule za msingi na sekondari pamoja na zahanati za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Valentino Hongoli, ambaye alimwakilisha Mbunge wa Jimbo la Lupembe, Edwin Swale, alimwambia waziri kuwa licha ya huduma ya umeme kufika sehemu mbalimbali katika jimbo hilo, bado kuna shule na zahanati hazina nishati hiyo.

Kwa upande wa Waziri Kalemani aliisisitiza TANESCO kuacha mara moja tabia ya kuwalipisha wananchi nguzo kwa sababu tayari serikali imeshatoa fedha.

"Kila mkoa tayari tumeleta fedha kiasi cha Shilingi bilioni 2.7 ambazo ni za nguzo sasa sitaki kusikia mnawatoza wananchi fedha kwa sababu serikali imegharamia," alisema Kalemani.

Pia aliwataka wenye viwanda vya kuzalisha nguzo nchini kuzalisha za zege ili kukabiliana na maeneo korofi.

# Taasisi zamgusa Meya D'Salaam kuchangia damu

**Na Mwandishi Wetu**

WANACHAMA wa Jumuiya ya Khoja Shia Ithna-Asheri Jamaat (KSIJ) kwa kushirikiana na Taasisi ya Ibrahim Hajj, wamejitolea kuchangia damu kwa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo cha Imamu Hussein.

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, alihudhuria hafla hiyo iliyofanyika Msikiti wa KSIJ jijini humo, ambako aliwapongeza wana Jumuiya hao kwa kudumisha utamaduni chanya wa kusaidia wenye uhitaji ikiwamo uchangiaji wa damu huo.

Meya Kumbilamoto alibainisha kuwa, KSIJ na Ibrahim Hajj, wameionyesha jamii ya Watanzania namna wanavyopaswa kujitoa kwa ustawi wa maisha wenye uhitaji, na kwamba damu iliyochangwa na wanajumuiya hao, inaenda kuokoa maisha ya wengi miongoni mwa wahanga wa ajali, wajawazito na wagonjwa wa kansa ya damu.

Kumbilamoto aliwapongeza KSIJ na Ibrahim Hajj na kuzitaka taasisi zingine na jamii kuiga utamaduni chanya unaofanywa na wanachama hao, ambao unalenga sio tu kuakisi yalivyokuwa maisha ya kiongozi wao Imamu Hussein, bali kuunga mkono jitihada za serikali katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wake.

"Nitoe wito kwa jamii, kuiga mfano wa KSIJ na Ibrahim Hajj, ambao wamekuwa wakijitolea damu kila mwaka. Awali walikuwa wakitoa mara moja kwa mwaka kila wanapokuwa na maadhimisho haya, lakini sasa wamekuwa wakichangia damu kila wanapoombwa kufanya hivi.

"KSIJ na Ibrahim Hajj, wameenda mbali zaidi kwa sasa kwa kujitosa katika utatuzi wa changamoto mbalimbali, hasa zinazoikabili sekta ya elimu na afya nchini, walikotoa vifaa tiba, vifaa vya elimu na hata ujenzi na maboresho ya miundombinu kwenye Sekta hizo muhimu kwa maendeleo ya jamii," alisisitiza Meya Kumbilamoto.

Akizungumza kwa niaba ya KSIJ, Ain Sharrif, mwanachama mwandamizi Jumuiya hiyo, alisema utamuduni huo wa kuchangia damu wamekuwa wakiufanya kila (Mwezi Muharram) wanapoadhimisha kifo cha kiongozi wao Sayyidina Hussein (Imamu Hussein), aliyekufa kwa kujitoa mhanga yapata miaka 1400 iliyopita.

"Tumekuwa tukifanya hivi tangu mwaka 2008, lengo likiwa ni kuyaishi maisha ya Imamu Hussein, ambaye alisimama imara katika kujitolea kwa ustawi wa maisha ya aliowaongoza na jamii iliyomzunguka. Nasi tunafanya haya na mengineyo ili kufuata nyayo zake na kutii wosia zake."

"Leo tunavyo vituo vitatu vinavyochangia damu jijini Dar es Salaam, ambapo pia kupitia Hospitali ya Ibrahim Hajj tumekuwa tukisaidia mamia ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu kwa kuwapatia misaada mbalimbali kulingana na mahitaji yao, sambamba na huduma za matibabu," alisema Sharrif.

## Taliban yataka wahudumu afya wa kike kurudi kazini

**Kabul, AFGHGHANISTAN**

TALIBAN imetoa wito kwa wahudumu wa afya wanawake Afghanistan, warudi kazini kuhudumu.

Zabihullah Mujahid, mmoja wa wasemaji wa Taliban, alitangaza kuwa wafanyakazi wa afya wa kike wa Wizara ya Afya, waliitwa kuendelea na majukumu yao katika ujumbe uliotolewa kwenye Twitter.

Mujahid, katika chapisho lake, alisisitiza kwamba utawala mpya hauna shida na wahudumu wa afya wa kike kuendelea na kazi zao. "Wizara ya Afya inawaarifu wafanyakazi wote wa kike katika majimbo na mji mkuu kuendelea na kazi zao," alitumia kifungu hicho.

Msemaji Mujahid aliwashauri wanawake Afghanistan wasiondoke nyumbani mpaka usalama utakaporejeshwa, akisema ni utaratibu wa muda.

Kuhusu wasiwasi kwamba Taliban itazuia uhuru wa wanawake Afghanistan, Mujahid alitangaza kwamba utawala mpya unaendelea na juhudi zake kuhakikisha kurudi kwa wafanyakazi wa umma wa kike kwenye kazi zao.

**TRT**

## Papa Francis atoa wito dunia kuiombea Afghanistan

**Vatican City, VATICAN**

PAPA Francis amesema wakristo duniani wafunge na kuomba na kumwomba Mungu kurejesha amani Afghanistan.

Papa ameyasema hayo jana kwenye misa ya Jumapili, eneo la St. Peter, akisema kuna wasiwasi mkubwa na mazishi yakiendelea kufuatia shambulio la kujitoa mhanga uwanja wa Kabul, wiki iliyopita.

"Ninaomba msaada uendelee kutolewa kwa wahitaji na kuomba ili mazungumzo yafanyike kwa ajili ya amani kwa nchi hapo baadaye, " alisema.

Zaidi ya watu 100 wakiwamo wanajeshi wa Marekani 13, waliuawa katika shambulio la bomu la kujitolea mhanga mjini Kabul Jumamosi.

Mshambuliaji aliendesha gari la kubebea wagonjwa na kupita kwenye kituo cha ukaguzi cha polisi hadi kwenye mtaa wenye umati wa watu katika wilaya yenye majengo mengi ya serikali na balozi.

Serikali ya Afghanistan ilitangaza Jumapili kama siku ya maombolezi, huku mazishi ya waathiriwa na msako wa manusura kwenye hospitari vikiendelea.

Kundi la Taliban la kiislam lenye itikadi kali lilitangaza kuwa lilitekeleza shambulio hilo.

**REUTERS**

# UNHCR yaokoa wahamiaji 130 pwani ya nchini Libya

**Tripoli, LIBYA**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limesema limewaokoa wahamiaji haramu 130 katika pwani ya Libya na kuwarejesha nchini humo.

"Watu 13 waliokolewa kwenye boti mbili ambazo zilizama katika bahari majira ya jioni na kurejeshwa Tripoli," liliandika shirika hilo kwenye ukurasa wake wa tweeter.

"Wanne kati yao walipotea. UNHCR pamoja na Shirika la Kimataifa la Msalaba Mwekundu (IRC) lilitoa msaada wa dawa, chakula na maji kwa waathiriwa na wengi wao walikuwa wana upungufu wa maji mwilini," lilisema UNHCR.

Libya imekuwa ikikabiliwa na hali ya usalama duni tangu kuangushwa kwa uongozi wa Muammar Gaddafi mwaka 2011, na kulifanya taifa hilo kuwa eneo la kuondokea wahamiaji haramu wanaokwenda nchi za Ulaya kupitia bahari ya Mediterranean.

Hadi mwaka huu zaidi ya wahamiaji hao wapatao 22,000 ikiwamo wanawake na watoto wameokolewa huku mamia wakipoteza maisha na baadhi kupotea kwenye ufukwe wa Libya, kwa mujibu wa Shirika la Uhamiaji la Umoja wa Mataifa (IOM).

XINHUA

Marekani yaonya shambulio lingine Afghanistan ndani ya siku tatu

Kabul, MAREKANI

MAREKANI imeonya kuwa kuna kitisho cha kuaminika karibu na uwanja wa ndege wa Kabul na imewataka raia wake kuondoka kwenye eneo hilo mara moja, taarifa iliyotolewa na ubalozi wa Marekani mjini Kabul, imesema jana asubuhi.

Ubalozi wa Marekani umewataka Wamarekani kuepuka kwenda kwenye uwanja wa ndege wa Kabul, pamoja na kutumia milango yote mikuu ya kuingilia katika uwanja huo.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema maeneo yanayopaswa kuepukwa ni pamoja na lango kuu la upande wa Kusini, wizara mpya ya mambo ya ndani na lango karibu na kituo cha mafuta cha Panjshir, kilichoko upande wa Kaskazini Maghabiri mwa uwanja huo wa ndege.

Wakati huohuo, Rais wa Marekani Joe Biden alisema kuwa shambulizi la vikosi vya Marekani ambalo liliwaua maofisa wawili wa kundi la Islamic State (IS) halitakuwa la mwisho.

Katika taarifa, Biden alisema Marekani itaendelea kuwasaka watu wote waliohusika katika mauaji yaliyotokea katika uwanja wa ndege wa Kabul na kuwachukulia hatua kali.

***RFI***




Watoto wakipumzika ndani ya nyumba iliyojaa maji Wilaya ya Morigaon Jimbo la Assam, Kaskazini Mashariki mwa India, juzi, baada ya eneo hilo kukumbwa na mafuriko. **PICHA: XINHUA**

# Somaliland kuwapokea wakimbizi wa Afghanistan

**Hargeisa, SOMALILAND**

BAADA ya Uganda wiki hii kupokea wakimbizi kutoa Afghanistan, pia Somaliland imesema imefungua milango kwa wakimbizi hao.

Tangu Taliban ichukue madaraka Agosti 15, mwaka huu, makumi ya maelfu ya Waafghan wanaondoka nchini humo.

Marekani ilitoa wito kwa jamii ya kimataifa kuwapokea kwa muda raia wa Afghanistan ambao bado wako kwenye makambi ya jeshi katika nchi zingine, kama Qatar.

Somaliland, eneo linalojitangaza kujitawala, imesema imejibu ombi la Marekani.

Kwa sasa, hayo ni makubaliano ya mawanzo. Jamhuri inayojitawala ya Somaliland ilielezea utayari wake wa kuwakaribisha wakimbizi wa Afghanistan, kwa muda tu, kwa kusubiri kusafirishwa katika nchi zingine kama Marekani.

"Kwa kweli mazungumzo yanaendelea kati ya Somaliland na maofisa wa Marekani, msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Somaliland aliliambia shirika la habari la AFP, akibainisha kuwa makubaliano hayo yako katika hatua ya mwanzo, na hakuna maelezo juu ya utaratibu wa kiufundi au tarehe za kuwasili ambazo zimewekwa, pia idadi ya wakimbizi husika haijajulikani bado.

Somaliland inawapa hifadhi wakimbizi maelfu kadhaa, hasa kutoka Ethiopia, Yemen na Syria.

Kufikia sasa kufungua mipaka yake kwa Waafghan, Hargeisa, inafuata nyayo za Kampala, ambayo tayari imepokea wakimbizi 51 ambao wanasubiri kupelekwa nchi nyingine.

Pia ni fursa kwa Somaliland kujiweka sawa kimataifa. Kwa sababu eneo hilo, lililojitangaza kujitawa kutoka Somalia mnamo mwaka 1991, halijatambuliwa rasmi. Mogadishu inalichukulia kama moja ya sehemu zake. Ingawa Hargeisa, ina serikali yake na inafanya uchaguzi wake mwenyewe.

***RFI***

MECHI KALI
HOME
AWAY
BROMLEY
2.07 | 3.60 | 3.35
EASTLEIGH

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money
tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
halopesa

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# ALLEGRI AITAKA JUVE KUMSAHAU RONALDO WAKATI IKILA KICHAPO

**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri, amesema Juventus haiwezi kuendelea kufikiria kuhusu Cristiano Ronaldo baada ya kuwa na wakati mgumu kwenye Serie A, wakati wakichezea kichapo kutoka kwa Empoli, wakiwa bila ya nyota huyo aliyetimkia Manchester United.

Juve ikiwa bila ya mfungaji wao huyo Ronaldo, anayekaribia kusaini kwa miamba wa Ligi Kuu England, Man United, walijikuta wakiangushiwa kichapo cha bao 1-0 na timu iliyopanda daraja, Empoli, juzi Jumamosi.

Bao la Mancuso liliinyanyua Empoli na kuibuka na ushindi huo wa kushangaza kwa Juve, ambayo wiki iliyopita ilitoka sare na Udinese kwenye mchezo wao wa ufunguzi wa ligi hiyo msimu huu.

Juve ilishindwa kupata ushindi katika mechi mbili za ufunguzi wa ligi hiyo kwa mara ya tatu katika misimu 52 ya Serie A iliyopita - wakifanya hivyo msimu wa 2010-11 na 2015-16.

Na kocha Allegri alipoulizwa kuhusu mshindi mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo kwa kuondoka kwake kumewapa changamoto, alijibu: "Cristiano alitumia miaka mitatu hapa Juventus, alifunga mabao, kitu ambacho ni kizuri sana, yeye ni mchezaji wa aina yake, lakini hatuwezi kufikiria kuhusu Ronaldo kwa sasa.

"Sina tatizo na kikosi, tunatakiwa tu kukubali kwamba, hatuwezi kutawala katika kila mchezo.

"Tunatakiwa kuwa pamoja na hilo litatusaidia kwenye mechi zetu zijazo na kwa majaliwa ya baadaye.

"Mara zote nina matumaini makubwa yakufanya vizuri, hivyo hilo si tatizo kwangu kwa wakati huu."

Ronaldo alijiunga na Juve kutoka Real Madrid mwaka 2018 na alikuwa mfungaji muhimu kwa miamba hao wa Italia, akitikisa nyavu mara 81 kwenye mechi 98 za Serie A.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alifunga mabao 29 msimu uliopita kwenye mashindano yote.




# *Tuchel alalamika kadi nyekundu kumharibia*

**LIVERPOOL, England**

THOMAS Tuchel amekubali maamuzi ya mwamuzi, Anthony Taylor, kumtoa nje kwa kadi nyekundu, Reece James wakati Chelsea ikitoka sare ya bao 1-1 na Liverpool, lakini amesema iliharibu mchezo wote pale kwenye dimba la Anfield.

Chelsea walikuwa mbele kwa bao moja huku wakionyesha mchezo wa kuvutia juzi Jumamosi likifungwa na Kai Havertz kwa kichwa.

Taylor aliridhishwa na maamuzi ya VAR baada ya mpira uliopigwa na Sadio Mane kuonekana umezuiwa kwa mguu na mkono na James ili usiingie nyavuni.

Na ikatolewa penalti iliyofungwa na Mohamed Salah katika kipindi cha kwanza, ingawa wachezaji wa Chelsea walionyesha kughadhabishwa na kadi nyekundu ya James.


Kikosi hicho cha Tuchel kilicheza kwa kipindi chote cha pili kikiwa na wachezaji 10 uwanjani, lakini kocha huyo raia wa Ujerumani anahisi mchezo huo uliharibiwa na kadi nyekundu.

"Kadi nyekundu - ambayo sifikiri kama ni sheria au si sheria, iliharibu mchezo," alisema akiambia BBC baada ya mchezo huo.

"Unatakiwa kukubali maamuzi, lakini pengine tungeweza kubadili akili yake kwa picha zinazotembea.

"Sipendi kadi nyekundu ya mapema kwa sababu iliharibu kabisa mchezo. Mwishoni mambo yalikuwa magumu na ilikuwa ngumu sana kupambana. Tulionyesha kiwango kizuri na tulistahili pointi."

Liverpool ilipiga mashuti 14 katika kipindi cha pili, sita kati yake yakiokolewa na golikipa, Edouard Mendy - akiwa ameokoa michomo mingi zaidi kwa mchezo mmoja wa Chelsea tangu alipojiunga nayo Septemba mwaka jana.



## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA






# MADRID KUACHANA NA MBAPPE

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid inaweza kuachana na mpango wa kuendelea kutaka kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa Le Parisien.

Madrid ilishatoa dau lao la euro milioni 190 kwa ajili ya kutaka kumsajili mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa.

Na kwa mujibu wa ripoti hiyo, Madrid sasa iliipa muda Paris St-Germain hadi kufikia jana Jumapili iwe imekubali dau lao.

Na kwamba, klabu hiyo ya Hispania haiko tayari kutoa ofa ya zaidi ya euro milioni 190 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Na kama Madrid itaachana na mpango wa kumsajili Mbappe katika dirisha hili la usajili wa majira ya joto linalofungwa kesho Jumanne, maana yake wanamsubiri atakapokuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Mbappe mkataba wake wa sasa na PSG unamalizika mwishoni mwa msimu huu na alikataa kuongeza mwingine mpya na klabu hiyo yenye maskani yake jijini Paris.

Na kama PSG hawakukubali kiasi hicho cha fedha hadi jana, maana yake Mbappe atabaki hapo Paris hadi mwishoni mwa msimu huu.

# Lewandowski amkuna kocha Nagelsmann

**MUNICH, Ujerumani**



KOCHA Mkuu wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, amepaza sauti kumsifia Robert Lewandowski, akimtaja kuwa ni mchezaji mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, baada ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' wakati wakiifumua Hertha Berlin mabao 5-0.

Lewandowski alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia katika mchezo huo wa Jumamosi, akifunga mabao hayo matatu na kuisaidia Bayern kuibutua vibaya Hertha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka, alifunga katika mechi yake ya 13 mfululizo kwenye Bundesliga - akiwa amezidiwa na marehemu Gerd Muller (aliyefunga mechi 16 mfululizo, msimu wa 1969-70) kuliko Lewandowski.

Lewandowski alifikisha mabao 301 kwa Bayern, katika mechi 333 na miamba hao wa Ujerumani, huku akishika nafasi ya pili nyuma ya Muller (mabao 566 mechi 607) katika historia ya klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, anashika nafasi ya pili kwa kufunga hat-trick nyingi zaidi (15) nyuma ya Muller (32).

"Kwa uhakika kabisa yeye ni mchezaji bora na mkubwa katika historia ya Bundesliga," alisema Nagelsmann akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Unatakiwa kupitia mengi, ligi imekuwa bora zaidi kwake, lakini yeye kiwango chake hakishuki amekuwa na uwezo mkubwa zaidi na kwa uhakika yeye ni bora zaidi."



MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 30 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3167 | Anyang vs Ansan Greeners | 1.90 | 3.10 | 4.07 |
| 14:00 | 2353 | Hermanstadt vs Miercurea Ciuc | 1.64 | 3.48 | 5.03 |
| 16:00 | 4779 | Anzhi Makhachkala vs FC Yessentuki | 1.05 | 10.67 | 21.34 |
| 17:00 | 1098 | Halifax vs Altrincham | 1.81 | 3.62 | 3.91 |
| 17:00 | 1282 | Dover vs Boreham Wood | 3.27 | 3.41 | 2.06 |
| 17:00 | 2212 | Bromley vs Eastleigh | 2.07 | 3.60 | 3.35 |
| 17:00 | 2304 | Barnet vs Dagenham and Redbridge | 3.18 | 3.42 | 2.09 |
| 17:00 | 4078 | Wealdstone vs Southend | 3.53 | 3.67 | 1.89 |
| 17:00 | 4258 | Welling vs Concord Rangers | 2.46 | 3.37 | 2.55 |
| 17:00 | 4409 | Aldershot vs Yeovil | 2.55 | 3.53 | 2.45 |
| 17:00 | 4524 | Kings Lynn vs Chesterfield | 3.13 | 3.52 | 2.08 |
| 17:00 | 4547 | Bradford PA vs Boston Utd | 5.40 | 3.85 | 1.62 |
| 17:00 | 5711 | Weymouth vs Maidenhead U | 2.35 | 3.32 | 2.78 |
| 17:00 | 5879 | Torquay vs Woking | 1.65 | 3.92 | 4.51 |
| 18:00 | 2867 | Clinceni vs CS Mioveni | 2.50 | 2.85 | 3.04 |
| 18:00 | 4099 | Parnu Jalgpalliklubi vs Tallinna Kalev | 11.88 | 7.72 | 1.17 |
| 18:30 | 2620 | Paide Linnameeskond vs FC Elva | 1.13 | 8.52 | 14.86 |
| 18:30 | 5067 | Floya vs Valerenga IF 2 | 2.33 | 3.83 | 2.47 |
| 18:30 | 5863 | Vifk Vaasa vs GBK Kokkola | 1.54 | 4.17 | 4.85 |
| 18:55 | 3253 | Proleter vs FK Radnicki 1923 | 1.78 | 3.47 | 4.05 |
| 19:00 | 4396 | Pors Grenland vs Stromsgodset 2 | 1.85 | 4.10 | 3.60 |
| 19:15 | 1499 | PKS Olimpia Elblag vs LKP Motor Lublin | 2.95 | 3.19 | 2.26 |
| 20:00 | 1334 | Nazareth Ilit vs Hapoel Katamon | 2.48 | 3.21 | 2.63 |
| 20:00 | 1708 | Hvidovre IF vs Hobro | 1.95 | 3.44 | 3.44 |
| 20:00 | 2143 | Odds BK 2 vs Notodden | 2.67 | 3.50 | 2.30 |
| 20:00 | 2958 | Mjondalen 2 vs Fredrikstad FK 2 | 1.72 | 4.15 | 3.67 |
| 20:00 | 3016 | Akropolis IF vs IFK Varnamo | 3.70 | 3.40 | 2.02 |
| 20:00 | 4478 | IFK Kumla vs IF Karlstad Fotbollutveckling | 1.76 | 3.97 | 3.63 |
| 20:00 | 5713 | Meppen vs TSV Havelse | 1.47 | 4.20 | 6.25 |
| 20:30 | 2825 | NewellS Old Boys vs Atletico Tucuman | 2.23 | 3.20 | 3.00 |
| 20:30 | 5178 | Union Santa Fe vs Argentinos Juniors | 2.66 | 2.81 | 2.76 |
| 21:00 | 1177 | FK Vozdovac vs Kolubara | 1.75 | 3.68 | 3.97 |
| 21:00 | 1294 | Mafra vs Vilafranquense | 1.71 | 3.58 | 4.51 |
| 21:00 | 2260 | Gaz Metan Medias vs UTA Arad | 2.94 | 2.89 | 2.54 |
| 21:00 | 2336 | AC Reggiana vs Aquila 1902 Montevarchi | 1.42 | 4.46 | 7.14 |
| 21:00 | 2601 | Justo Jose De Urquiza vs UAI Urquiza | 2.66 | 3.05 | 2.56 |
| 21:00 | 3098 | Flamengo RJ U20 vs Fluminense RJ U20 | 1.76 | 3.48 | 4.16 |
| 21:00 | 3467 | Tindastoll W vs Keflavik W | 2.14 | 3.62 | 2.85 |
| 21:00 | 5315 | Ferrocarril Midland vs Ituzaingo | 2.84 | 2.74 | 2.65 |
| 21:30 | 5121 | Wrexham vs Notts County | 2.10 | 3.81 | 2.88 |
| 21:35 | 1639 | Belgrano Cordoba vs Chacarita Juniors | 1.65 | 3.35 | 5.24 |
| 21:45 | 3680 | Sportivo Ameliano vs Fernando Mora | 2.32 | 3.08 | 2.94 |
| 22:00 | 1625 | Potenza SC vs Bari | 3.96 | 3.41 | 1.91 |
| 22:00 | 2489 | Boca Unidos vs Douglas Haig | 1.86 | 3.00 | 4.44 |
| 22:00 | 4457 | Le Mans vs Sete 34 FC | 2.12 | 3.03 | 3.52 |
| 22:45 | 3386 | San Lorenzo vs Patronato Parana | 2.51 | 2.94 | 2.80 |
| 23:00 | 1448 | Zaragoza vs FC Cartagena | 2.13 | 2.91 | 3.80 |
| 23:00 | 4915 | Valledupar FC vs Bogota FC | 1.79 | 3.35 | 4.21 |
| 23:15 | 1044 | Union Magdalena SM vs Real Cartagena | 1.64 | 3.54 | 4.97 |
| 23:15 | 1609 | CD Trofense vs Penafiel | 3.23 | 3.13 | 2.19 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG SASA ALIA NA WACHEZAJI ARSENAL

●●● Tunatakiwa kuzungumza na kusema ukweli kati yetu na kila mmoja, kuinua kiwango chetu...

**MANCHESTER, ENGLAND**

PIERRE-Emerick Aubameyang amewataka wachezaji wa Arsenal kuungana pamoja kama wanataka 'kuinua kiwango' baada ya kichapo cha mabao 5-0 kutoka kwa Manchester City, Jumamosi na kuwaacha bila pointi kwenye Ligi Kuu England.

Wakiwa tayari walishafungwa na Brentford na Chelsea katika mechi mbili za ufunguzi wa Ligi hiyo msimu huu wa 2021-22, 'Washikabunduki' hao wamekumbana na wakati mgumu na sasa wanachungulia kwenye mstari wa kushuka daraja baada ya kichapo cha Jumamosi.

City walifunga mara mbili ndani ya dakika 12 za mwanzo za mchezo huo, wakati Arsenal walikuwa na wachezaji 10 uwanjani baada ya Granit Xhaka kuonyeshwa kadi ya njano ya moja kwa moja sababu ya kucheza faulo.

Wamefungwa kuelekea wiki ya mechi za kimataifa, wakati ambao nahodha Aubameyang anaamini kikosi kinatakiwa kujitathmini na wachezaji kuzungumza kati yao wenyewe, wakiwa wamecheza vibaya sana dhidi ya kikosi cha kocha, Pep Guardiola pale kwenye dimba la Etihad.

"Tunatakiwa kuchukua jukumu na kuwa imara na mpira, na hatukufanya hivyo leo (juzi)," alisema Aubameyang.

"Baada ya hapo na kadi nyekundu kwa hakika mchezo ulibadilika kabisa.

"Lakini kama nilivyosema, hiyo haitoshi na kila mmoja sasa anatakiwa kuinua kiwango chake, tujiangalie sisi wenyewe kwenye kioo na kazi tunayofanya, hatuchezi kama timu na tunatakiwa kujikita pamoja na hii ndio njia pekee ya kusonga mbele.

"Tunatakiwa kucheza kwa ari na kujituma na hiyo ndio staili ya mchezo wetu, tunatakiwa kucheza kwa kujituma.

"Tunatakiwa kuchukua jukumu hili kama timu kwa wachezaji wote, tunatakiwa kujitoa kwa hali na mali kwa sasa.

"Nafikiri tunatakiwa kuzungumza kati yetu sisi wachezaji.

"Nafikiri ni muhimu kwa sasa kwa sababu sisi ni Arsenal na tunahitaji kujisikia fahari. Ni hivyo tu.

"Tunatakiwa kuzungumza na kusema ukweli kati yetu na kila mmoja, kuwa wamoja na kuinua kiwango chetu."

Aubameyang alifunga mabao matatu 'hat-trick' katikati ya wiki kwenye mchezo wa Kombe la EFL wakati wakiifumua West Brom mabao 6-0 kabla ya mchezo wa juzi wa Ligi dhidi ya Man City.

## ZISIKUPITE

### RONALDO NA REKODI YA MSHAHARA
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atakuwa ndiye mchezaji anayelipwa mshahara wa juu zaidi katika historia ya Ligi Kuu England, wakati atakapo kamilisha uhamisho wake kutoka Juventus kutua Manchester United. ***(Telegraph)***

### BEI YA KOUNDE YAPANDA
MATUMAINI ya Chelsea ya kumsajili Jules Kounde kutoka Sevilla yamefifia baada ya klabu hiyo ya Hispania kupandisha dau la kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 hadi pauni milioni 68.5 ***(Telegraph)***

### MBAPPE NA REAL MADRID
REAL Madrid imeipa Paris St-Germain hadi kufikia jana Jumapili iwe imekubali dau lao kwa ajili ya mshambuliaji wao Kylian Mbappe, kwani klabu hiyo ya Hispania haiko tayari kutoa ofa ya zaidi ya euro milioni 190 kwa jili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Le Parisien)***

### UNITED YAKOMAA NA TRIPPIER
KLABU ya Manchester United imepanga kufanya uhamisho wa muda wa mwisho kwa beki wa England mwenye umri wa miaka 30, Kieran Trippier, huku Atletico Madrid ikisemekana kuhitaji malipo ya pauni milioni 34.3 kwa ajili ya mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham**. *(AS via HITC)***

### DORTMUND YAMTAKA DALOT
BORUSSIA Dortmund ina matumaini ya kumsajili beki, Diogo Dalot raia wa Ureno kutoka Manchester United iwapo klabu hiyo ya Ligi Kuu England itaweza kupata mchezaji atakayechukua nafasi ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMUWANIA EMERSON
TOTTENHAM Hotspur imeanza juhudi za kumsaka beki wa kulia wa Barcelona, Emerson Royal mwenye umri wa miaka 22, na kumwachia, Serge Aurier, 28, kutasaidia juhudi zao za kumsajili raia huyo wa Brazil. ***(Telegraph)***

### KEAN MIAKA MIWILI JUVE
JUVENTUS wanakamilisha shughuli ya kumsainisha mkataba mshambuliaji Muitalia Moise Kean ambaye amesaini miaka miwili ya mkopo kutoka klabu ya Everton, kwa sharti la kumnunua moja kwa moja mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ambaye alijiunga na Toffees hao mwaka 2019. ***(Sky Sports)***

### WOLVES SAFI KWA HEE-CHAN
WOLVES wanakaribia kukamilisha kumsajili mshambuliaji wa Korea Kusini, Hwang Hee-chan kutoka RB Leipzig. Huku klabu kama vile Brighton, West Ham na Atalanta pia zikiwa miongoni mwa zilizomtaka Chan mwenye umri wa miaka 25 msimu huu. ***(Telegraph)***

### MAITLAND-NILES KUTUA EVERTON
EVERTON wanataka kumsajili beki, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 23, kwa mkopo kutoka Arsenal. ***(Sky Sports)***

### PALACE YAMWANIA EDOUARD
KLABU ya Crystal Palace imetoa ofa ya dau la pauni milioni 15 kwa ajili ya kumsajili Mfaransa anayechezea klabu ya Celtic, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail).***

## Tiger yamnasa Kocha Mkenya

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

UONGOZI wa Tiger Queens, itakayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, imeingia mkataba na Kocha Mkuu wa Mabingwa wa Ligi ya Kenya, Vihiga Queens, Alex Alumira kwa ajili ya msimu ujao wa wa 2021/22, imefahamika.

Tiger Queens itashiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa mara ya kwanza baada ya kuinunua Kigoma Sisterz ambayo imefikia uamuzi wa kuiuza timu yao.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Mmiliki wa Tiger Queens, Potin David Pelo, alisema ameingia mkataba wa miaka mitano na kocha huyo raia wa Kenya na anaamini atasaidia kuongeza ushindani kwenye Soka la Wanawake Tanzania.

Potin alisema kocha huyo ataanza ajira yake mpya baada ya kumalizika kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA inayoendelea jijini hapa.

"Tumeshakamilisha mazungumzo yote na Alumira, ninaamini atatusaidia kufika katika malengo yetu, tunataka kuingia na makali katika Ligi Kuu ya Wanawake msimu ujao," alisema Potin.

Kwa upande wa Alumira alisema: "Ninafuraha kubwa kuja Tanzania, nitaongea zaidi nikifika huko, kwa sasa namalizia kazi ya Vihiga Queens."

## Mayanga apewa malengo Prisons

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Tanzania Prisons, umesema malengo makubwa ambayo wamempa Kocha Mkuu wao, Salum Mayanga, ni kuhakikisha timu hiyo inamaliza msimu katika nafasi sita za juu kwa msimu huu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Septemba 29, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Mkwanda Mkwanda, alisema wameshakamilisha usajili wa wachezaji wapya kwa asilimia 95 na timu hiyo itaingia kambini leo kuanza maandalizi lengo likiwa ni kufikia malengo hayo.

Alisema tayari wamekutana na benchi la ufundi linaloongozwa na Mayanga na kumpa vipaumbele vyao kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo ambayo msimu huu itashirikisha timu 16 kutoka 18 za msimu uliomalizika.

"Msimu huu utakuwa mgumu na ushindani mkubwa ukizingatia hizi fedha zilizotolewa na mdhamini mpya (Azam Media), zinachangia kwa kila kitu kujipanga vizuri. Baada ya kukamilisha usajili wetu tulikutana na kocha kumweleza mikakati yetu kutokana na msimu uliopita kumaliza nafasi ya saba sasa tunahitaji kupanda juu," alisema.

# NDAYIRAGIJE AAHIDI KUIPAISHA GEITA GOLD

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

KOCHA Mkuu mpya wa Geita Gold FC, Ettiene Ndayiragije, amesema uhusiano mzuri alionao na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Felix Minziro, kabla hata ya kujiunga na timu hiyo, anaamini utawasaidia kwa pamoja kuiwezesha klabu hiyo kufikia malengo yake.

Ndayiragije ambaye kabla ya kutua katika klabu hiyo amewahi kuinoa, Mbao FC, KMC FC, Azam FC na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars na kusaidia kufuzu michuano ya CHAN mwaka 2019, amesema hana tatizo kufanya kazi na Minziro ambaye ameipandisha Ligi Kuu klabu hiyo.

Akizungumza na gazeti juzi, Ndayiragije alisema si mara ya kwanza kufanya kazi na mwalimu huyo japo haikuwa moja kwa moja, kwani wakati anaichukua timu ya KMC yeye ndiyo alikuwa anaondoka.

"Namfahamu sana na ni mtu ambaye nipo naye karibu, kabla sijafika hapa nilikuwa nazungumza naye kwa hiyo ushirikiano ulikuwapo na utaendelea kuwapo kwa sababu tunaongea lugha moja, na tunamwomba Mungu atuepushe na ibilisi.

"Kwa upande wangu sina shida na ninaamini pia katika utendaji wake, tutafanya mambo makubwa na sina mpango wa kutafuta kocha msaidizi mwingine," alisema Ndayiragije.

Kuhusu kikosi hicho tangu ajiunge nacho, Ndayiragije amesema amewaona vijana wake na ni wenye vipaji na wana vitu vingi, lakini wanahitaji uzoefu wa Ligi Kuu na kuongezewa mbinu jambo ambalo wakilitekeleza kwa umakini wanaweza kufanya kitu kikubwa na kufika mbali.

"Kwa ujumla timu ipo vizuri sana kuanzia wachezaji mpaka viongozi, tunaendelea kufanya kazi na wachezaji wanaendelea kubadilika polepole na kutokana na uhalisia wa Ligi Kuu nina imani wataimarika sana na kufika mbali," alisema.

Kwa upande wa usajili, kocha huyo alisema kwa muda uliobaki ni vigumu kwake kutoa mapendekezo kwa sababu wameshakamilisha idadi inayotakiwa, lakini yeye simuumini wa kusajili sana kwani hupenda kuamini wachezaji waliopo.

"Jambo la kwanza ni kuwajenga kisaikolojia ili kujua Ligi Kuu inahitaji nini na kipi tufanye katika ligi hiyo, kwa hiyo suala la ufundi au kipaji uwanjani ninaona wengi wanacho na wapo kabisa vizuri, lakini tatizo kubwa linakuwa ni kujiandaa kujua unaenda kufanya nini na unakutana na nani," alisema.




Mshambuliaji wa Simba Queens, Mkongomani Flavine Mawete (kushoto), akimtoka beki wa PVP FC ya Burundi katika mechi ya Kundi A iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyayo jijini Nairobi, Kenya juzi. Simba Queens ilishinda mabao 4-1. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Kocha achambua ushindi Simba Queens CECAFA*

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

LICHA ya kupata ushindi mnono katika mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Ukanda wa CECAFA, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, amesema mechi dhidi ya wapinzani wao, PVP FC kutoka Burundi haikuwa nyepesi.

Simba Queens iliichapa PVP FC mabao 4-1 wakati kinara wa Kundi A ni mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Uganda, Lady Doves iliyowatandika FAD ya Djibouti mabao 5-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini hapa jana, Hababuu alisema timu yake haikuonyesha kiwango kizuri hasa katika kipindi cha kwanza, hivyo alilazimika kufanya mabadiliko mapema ili kuimarisha kikosi chake.

Hababuu alisema PVP iliwasumbua, lakini alilazimika kubadilisha mbinu kwa ajili ya kufanikisha wanaondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo huo wa ufunguzi.

" Mechi haikuwa rahisi kama ambavyo tulitarajia, tulikutana na mabingwa wenzetu, wote tumekuja kupambana, hivyo nililazimika kufanya uamuzi wa kumbadilisha kipa baada ya kuona amefanya makosa mawili ambayo yalitugharimu," alisema Hababuu.

Kocha huyo alisema wataendelea kujipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi za hatua ya makundi zilizobaki ili kuhakikisha wanasonga mbele na hatimaye wanatimiza malengo ya kukata tiketi ya kushiriki fainali za Afrika.

"Tunaendelea kujipanga kuhakikisha tunapata kile tulichokifuata, haya ni mashindano makubwa na kila mchezaji anataka kuonyesha uwezo wake wa kucheza, Simba yote malengo ni moja, ile ya wanaume, vijana na hawa wanawake," alisema.

Mabao ya Simba Queens katika mechi ya juzi yalifungwa na Danai Bhobho, Aisha Juma na Mkongomani Flavine Mawete, ambaye alicheka na nyavu mara mbili.

Simba Queens itashuka tena dimbani kesho, Jumanne kucheza dhidi ya Lady Doves wakati PVP itawakaribisha FAD.

# Michezo

Jumatatu Agosti 30, 2021
Nipashe



Aubameyang alia na wachezaji Arsenal UKURASA 22




Mashabiki wa Yanga wakiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia tamasha la Kilele cha Wiki ya Mwananchi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HAIJAWAHI KUTOKEA

## ●●● Dar yasimama na kugeuka kijani na njano, ni zaidi ya mafuriko kwa Mkapa huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HAIJAWAHI kutokea! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na tamasha la tatu la Yanga la Kilele cha Wiki ya Mwananchi kufunika mwanzo mwisho kwa kila kitu kuanzia mahudhurio, burudani na namna utambulisho wa wachezaji ulivyo fanywa.

**Katika tamasha hilo lililofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ambalo ni mara ya tatu kwa Yanga kuadhimisha tangu ilipofanya kwa mara ya kwanza mwaka 2019, lilifana zaidi na kujaza pengine kuliko matukio yote yaliyowahi kufanyika uwanjani hapo tangu umeanzishwa.**

Wanayanga na viongozi wote waliohudhuria kilele hicho, wakiongozwa na mgeni rasmi Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah.

Mbali na utambulisho wa wachezaji hao, wanachama na mashabiki walipata burudani mbalimbali kutoka kwa wanamuziki na wasanii mbalimbali nchini, akiwamo mwanamuziki maarufu Afrika, Koffi Olomide, ambaye aliburudisha kwa nyimbo zake za miaka ya nyuma zilizompatia umaarufu kama 'Loi', na za miaka ya karibuni kama 'Selfie' na 'Papa Ngwasuma', maarufu kama 'Papa Mobimba.'

Mmoja wa wasemaji wa klabu hiyo aliyejiunga na klabu hiyo hivi karibuni, Haji Manara, aliwatangaza na kuwaita wachezaji 27 watakaoichezea klabu hiyo kwa msimu ujao wa michuano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

### KUWASILI KWA TIMU

Kikosi cha Yanga kiliingia uwanjani saa 9:28 alasiri kwa basi lao jipya, huku wachezaji na benchi la ufundi wakiwa wamevalia suti ya rangi ya kijivu.

Wakati wachezaji wote walishuka kwenye basi na kuingia kwenye vyumba vya kubadili nguo, kasoro mshambuliaji, Yacouba Songne, ambaye aliingia na Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Yanga, Hersi Said. Mwitikio wa mashabiki ulikuwa mkubwa tofauti na matamasha yote ya Kilele cha Wiki ya Mwananchi na hata kuzidi maudhurio ya mechi Yanga ilizowahi kucheza katika uwanja huu, ambapo jana maeneo ya Taifa yalianza kupendeza tangu saa1:00 asubuhi kwa rangi ya kijani na njani kutamba kila kona.

### MBWEMBWE ZA MANARA

Saa 11:30 Manara aliingia uwanjani na kuzua shagwe ndani ya uwanja akizunguka uwanja na kuwasalimia mashabiki wa timu hiyo akiwa na jezi ya Yanga.

Manara alitokea uwanjani baada ya MC, Maulid Kitenge, alipomuita mchezaji Ditram Nchimbi kwa ajili ya kutambulishwa nyota huyo hakutokea na baadaye kutoka aliyekuwa msemaji wa Yanga.

Baada ya kutambulishwa Manara akapewa kipaza sauti kwa ajili ya kuwatambulisha wachezaji wapya wa msimu huu ambapo aliwapamba kwa kila aina ya mbwembwe huku akishangiliwa na maelfu ya mashabiki uwanjani hapo.

### NYOTA WALIOTAMBULISHWA

Wachezaji hao ni Djigui Diara, Ramadhani Kabwili, Erick Johora. Djuma Shaaban, Kibwana Shomari, David Brayson, Adeyum Suleiman, Yassin Mustapha, Abdallah Shaibu 'Ninja', Dickson Job, Bakari Mwamnyeto na Yanick Bangala.

Wengine ni Mukoko Tonombe, Deus Kaseke, Feisal Salum 'Fei Toto", Zawadi Mauya, Saido Ntibazonkiza, Farid Mussa, Balama Mapinduzi, Ditram Nchimbi, Dickson Ambundo, Fiston Mayele, Heritier Makambo, Yacouba Songne, Yusuph Athumani, Jesus Moloko na Paul Geofrey.

Hata hivyo, mchezaji ambaye hakuwapo kwenye kikosi hicho ni Khalid Aucho, ambaye amekwenda kuitumikia timu yake ya Taifa, Uganda Cranes.

### YANGA PRINCESS YANOGESHA

Pamoja burudani mbalimbali mashabiki walishuhudia mechi ya kwanza ya Yanga chini ya miaka 20, wakikubali kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Cambiaso inayofundishwa na kocha wa zamani wa Mtibwa Sugar na Kagera Sugar, Mecky Mexime, huku kikosi cha timu ya Wanawake, Yanga Princess kikilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ilala Queens.

### MKUU MKOA DAR

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akielezea alivyopokea tamasha hilo, alisema amefurahishwa na kuwapongeza Yanga kufanya shughuri za kijamii ikiwamo kuhamasisha suala la kupata chanjo.

"Hakuna mtu asiyejua mapenzi yangu kwa timu ya Simba, hili tamasha limekuwa la kipekee, kwa sababu wamefanya shughuli mbalimbali za kijamii na isotoshe mashabiki wao kujaza uwanja na kuchangia Mkoa wa Dar es Salaam kuingiza mapato.

"Nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, najivunia sana uwapo wa hizi klabu pamoja na timu zingine, niwahakikishie pia kwenye tamasha la Simba [Simba Day] nitakuwapo," alisema Makalla.

### MECHI DHIDI YA ZANACO

Baada ya shughuli zote kufanyika, ilifuata mechi ya Yanga na Zanaco ya Zambia, ambayo mashabiki wa Wanajangwani hao walishuhudia nyota wao wapya wakiichezea timu hiyo kwa mara ya kwanza, lakini hadi gazeti hili linakwenda mitamboni timu hizo zilikuwa hazijafungana.

Yanga itaingia tena kambini kujiandaa na mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Septemba 10-12, dhidi ya Rivers United ya Nigeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kabla ya marudiano nchini Nigeria Septemba 17, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >